Jumamosi Aprili 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579897

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



## Ajali za Coaster, UDART zilivyoua Mwanza, Dar

UKURASA 3




Kumbe Pam D unaheshimu mashabiki!

UKURASA 13

# Makanisa yaonya njaa

• **Ni** kutokana na kukosekana mvua, viongozi waonywa kutowaonea wanyonge... *Ukurasa 2*



Waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Azania Front, wakiigiza mateso ya Yesu Kristo, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu kanisani hapo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## W'biashara mifuko plastiki waomba miezi 8



UKURASA 2

MIKOPO YA WATUMISHI:

## Ripoti ya CAG yanusa uonevu kwenye makato

UKURASA 3

SPECIAL FEATURE ON INDUSTRIALIZATION DEVELOPMENT IN TANZANIA

"NCHI YA VIWANDA"





**The Guardian Ltd,** wish to inform the public and our esteemed Clients that, A special feature on Industrialization in Tanzania which was supposed to be published on **18th April 2019** was put on hold to **23rd April 2019.**

**We apologise for inconvenience caused.**

**We wish you all a good Easter Holiday**

**Contact Supplement Coordinators**

**Moses Masunga,**
**Email:moses.masunga@guardian.co.tz,**
**Phone No.0755 642851,**

**Charles Masele,**
**Email:masele7@gmail.com,**
**Phone No.0789 637363.**

The Guardian Nipashe CTI

## W'biashara mifuko plastiki waomba miezi 8

**Na Mary Geofrey**

WAKATI serikali ikiwa imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia Juni Mosi mwaka huu, wafanyabiashara wa mifuko hiyo jijini Dar es Salaam, wameiomba kuwapa miezi nane ili kumaliza kuuza bidhaa zao.

Wameisihi serikali kuwapa muda huo ili wamalize kuuza bidhaa walizokuwa wameshanunua kutoka viwandani zimalizike ili kuepuka kupoteza mitaji yao.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabishara wa Kariakoo wanaouza mifuko ya plastiki, Ramadhani Mussa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tunaunga mkono juhudi za serikali katika kuanza kutumia mifuko mbadala, lakini ombi letu kabla ya muda uliowekwa na serikali, tunaomba sisi wafanyabiashara tupewa miezi nane hadi itakapofika Desemba, mwaka huu, ili tumalize bidhaa tulizonazo," alisema Mussa.

Alisema bado wana akiba nyingi ya mifuko hiyo na tangu kutolewa kwa tamko la usitishwaji mifuko hiyo, biashara imeshuka kwa asilimia 80 kutokana na wateja kuacha kununua mifuko hiyo.

"Kutokana na kuwapo kwa changamoto ya kukosa wateja, tunaiomba serikali utuongeze muda ili hii tuliyonayo iishe kwanza kwa ajili ya kuokoa mitaji yetu," alisema.

Naye mwanachama wa jumuiya hiyo, Abimu Mlidwa, alisema kuongezewa kwa muda kutasaidia kulinda mitaji yao kwa sababu soko la bidhaa hiyo limeshuka kutoka kuuza katoni 20 kwa siku hadi kufikia kuuza katoni moja kwa siku.

Aprili 9, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akijibu hoja za wabunge waliochangia mjadala wa kupitisha bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka fedha 2019/2020, alitangaza kuwa kuanzia Juni Mosi, 2019, itakuwa ni mwisho wa kutumia mifuko ya plastiki nchini.

Katazo hilo la uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki kwa lengo la kuzuia uchafuzi wa mazingira, linaendana na lile la nchi za Kenya na Rwanda ambazo zilizuia matumizi ya mifuko hiyo miaka kadhaa iliyopita.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Lazaro Mambosasa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuimarisha ulinzi na usalama kwa kipindi hiki cha sikukuu ya Pasaka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makanisa yatahadharisha njaa

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Mhashamu Isaack Amani, amewataka Watanzania kuhifadhi chakula, kutokana na kukosekana kwa mvua za masika ili kujikinga na janga la njaa.

Akitoa ujumbe wa Ijumaa Kuu jijini hapa jana, katika maadhimisho ya Ibada ya Umoja wa Makanisa ya Kikristo mkoani Arusha, Askofu Mkuu Amani, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Umoja huo, alisema, mvua za masika hazijanyesha, hivyo, ni vema kila mtu akachukua tahadhari.

"Nninawaasa, ni vema kila mtu akaona hili ni tatizo, chukueni hatua kwa kuhifadhi chakula ili mwakani hali za kifamilia zisiwe mbaya zaidi," alisema.

Alisema hali ya ukosefu wa mvua inatokana na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti ovyo bila kurudishia.

Askofu Amani alitoa mfano Ulaya kila mlima umezungukwa na msitu wa miti, tofauti na nchini ambapo milima mingi haina miti, hali inayochangia kutoweka kwa mvua.

"Nawaomba kila mmoja aweke bidii kuotesha miti ili tuondokane na janga la ukosefu wa mvua ambayo inatupa neema ya chakula na kila kitu," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa Watanzania kujenga utamaduni wa kukata bima ya afya kwa faida yao na familia zao pale wanapopatwa na magonjwa mbalimbali.

Alisema watu wengi wanapoteza maisha kwa kukosa fedha za kufanyiwa uchunguzi pale wanapohitajika au kununua dawa, hivyo njia pekee ya kuepukana na janga hilo ni watu kubadilika na kukata bima za afya.

Pia aliwataka watu kubadilika kwa kuishi maisha ya kumpendeza Mungu kwa kuepuka kufanya uzinzi ili kuepukana na ugonjwa wa Ukimwi.

"Lakini inasikitisha kuona siku hizi mpaka watoto wadogo wanajiingiza katika uzinzi sasa, tunajiuliza hawa wanajuaje mambo haya au sababu ya mitandao yetu, hivyo tubadilike," alisema.

Askofu Amani alisisitiza watu kuepukana na ulevi ambao umekithiri kwa baadhi ya watu na kuishi kwa upendo, uhuru na mshikamano.

**WAOMBEA AMANI, MSHIKAMANO**

VIONGOZI wa madhehebu mbalimbali mkoani Dodoma wamewataka Watanzania kudumisha amani na mshikamano nchini na kuishi maisha ya kumpendeza Mungu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana katika Ibada ya Ijumaa Kuu, Askofu wa Kanda ya Kati wa Kanisa la PHAM, Julius Bundala, aliwataka kudumisha amani na upendo miongoni mwa Watanzania kwa kuwa hata Rais John Magufuli amekuwa akisisitiza umuhimu wa amani nchini.

"Ni muhimu waumini

INAENDELEA UK. 8

# Askofu aonya viongozi wanaowaonea wanyonge

**Na Mary Geofrey**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe mkoani Kagera, Dk. Benson Bagonza, amewaonya viongozi wa serikali na dini wasiokemea maovu na wanatumia nafasi zao kuwaonea wanyonge na kujinufaisha wao binafsi.

Amewataka kuacha kutumia ukimya wa wanyonge kama mtaji wa kujinufaisha na mambo yao binafsi, kwa sababu ghadhabu yake itaipata vizazi vijavyo.

Askofu Bagonza aliyaeleza hayo jana, katika ibada ya Ijumaa Kuu ya kukumbuka mateso na kifo cha Yesu Kristo, zaidi ya miaka 200 iliyopita iliyofanyika katika Kanisa la KKKT, Dayosisi ya Karagwe, Usharika wa Kanisa Kuu la Lukajange.

Alisema Yesu Kristo alikubali kuvua ukuu wake, akateswa, akasulubiwa na kutundikwa msalabani kwa ajili ya watu wote wenye dhambi, lakini baadhi ya watu, viongozi wa serikali na dini, hawataki kuiga maisha yake bali wamekuwa sehemu ya kuwatesa wengine.

"Unyonge wetu, ukimya wetu na kuyafumbia macho maovu yanayofanywa si mtaji wa wasaka tonge, wanaojitolea kwa ajili ya maslahi yao binafsi kumwaga damu za watu na kuwaonea, wafahamu dhambi hiyo inadumu vizazi hadi vizazi," alisema Askofu Bagonza.

Aliwataka Watanzania kujitoa kwa ajili ya wengine, lakini si kuwakandamiza kama alivyofanya Yesu kufa kwa ajili ya watu wenye dhambi.

"Tujitoea kwa ajili ya watu wengine kwa sababu ni jambo ambalo linapotea ndani ya Kanisa la leo na Taifa. Kama tukifanya haya kwa kufuata maandiko ya neno la Mungu na uzalendo wa kuipenda nchi yetu, tutaishi kwa amani na upendo," alisema.

Alisema Watanzania wabadilike na kuonyesha tofauti ya watumwa na watu waliokombolewa na ambao hawajakombolewa kwa kuacha kufurahi kuona wengine wakiwa utumwani.

Alimtolea mfano Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kuwa baada ya kuona Taifa limepata uhuru alitumia rasilimali nyingi kuhakikisha anasaidia mataifa mengine kupata uhuru.

"Pia Mwalimu Nyerere alilifanya Taifa kuingia gharama kubwa kupinga udikteta ulipoingia katika nchi jirani kwa sababu aliona uhuru wa nchi hauna maana kama nchi nyingine hazina uhuru na sisi tunapaswa kuishi maisha haya," alisema Askofu Bagonza.

**AONYA MATUMIZI TEHAMA**

Katika ibada ya maadhimisho ya Ijumaa Kuu Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph jijini Dar es Salaam, Padri Novatus Mbaula, aliwakumbusha waumini namna teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehana) inavyosababisha watu kutenda dhambi na kumsahau Mungu.

"Leo hii hatuitaji kwenda mlima mrefu kama Yesu Kristo alivyopelekwa na shetani kwenda kuona mambo anayotendeka duniani, sasa hivi shetani anamwambia mwanadamu fungua simu utakuta utapeli wa fedha, unaambia ile fedha tuma huku, wanaotuma ni watoto wenu," alisema.

Padri Mbaula alisema unaku

INAENDELEA UK. 8

## HABARI ZA KITAIFA



Mfanyabiashara mdogo akiwa amejificha chini ya meza yake ya biashara katika eneo la Mnazi Mmoja, akijikinga na mvua zilizonyesha, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Wasiojulikana wapora kamera mbili za NIDA

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

KAMERA mbili za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) zimeibwa na watu ambao hadi sasa hawajafahamika wilayani Kahama Mkoa wa Shinyanga.

Hata hivyo Jeshi la Polisi limesema halijawa na uhakika kama waliohusika ni watu kutoka nje ya Nida, isipokuwa inawezekana kuwa wahusika ni watumishi. Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, akizungumza jana na Nipashe kwa njia ya simu, alikanusha madai kuwa ofisi zilivunjwa kabla ya wizi huo, lakini alithibitisha kuhojiwa kwa baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo.

Kamanda huyo alisema kuna tuhuma za watu wa ndani na siyo wizi wa mtu wa nje kama madai yanavyoeleza kuwa ofisi zilivunjwa kisha kamera hizo kuibwa.

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Abwao alisema Polisi wameamua kufungua jalada la uchunguzi kwa ajili ya kubaini ukweli juu ya upotevu wa kamera na kuongeza kuwa mahojiano yanaendelea na iwapo ukweli utapatikana, taarifa sahihi zitatolewa taarifa.

"Siyo kwamba kuna wizi wa mtu wa nje, bali ni vifaa kwenye pakeji walivyokabidhiwa inaonekana kamera hazionekani, hivyo tumefungua jalada la uchunguzi dhidi ya tuhuma hizo... nikwambie tu baada ya uchunguzi taarifa kamili nitakupatia," alisema Abwao.

Katika hatua nyingine, Abwao alisema matukio ya uhalifu hususan uvunjaji wilayani Kahama yameshika kasi na kuwa jumla ya watu 32 wamekamatwa katika operesheni maalum.

"Watu hao wamekamatwa kuanzia juzi kwenye operesheni huko Kahama, ambayo inaendeshwa na Mkuu wa Kitengo cha Upelelezi Mkoa wa Shinyanga na sasa Mji wa Kahama na wilaya kwa ujumla sasa upo shwari," alisema Abwao.

# CAG Assad anusa uonevu makato watumishi wa umma

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini kukiukwa kwa sheria na mwongozo wa serikali katika makato ya mishahara ya watumishi wa umma kurejesha mikopo waliyochukua kwenye taasisi za fedha.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, Prof. Assad anasema, amebaini kukiukwa kwa Kifungu namba tatu (3) cha Sheria ya Kurejesha Madeni ya Mwaka 1970.

Kifungu hicho kinaeleza kuwa ikitokea ofisa yeyote anadaiwa, pasipo kuwa na upendeleo wowote ule, mamlaka inayohusika na ofisa huyo inaweza kutafuta njia ya kurejesha deni hilo kwa kuruhusu ofisa huyo akatwe kidogo kidogo katika mshahara wake kila mwezi kwa kiasi kisichozidi robo moja ya mshahara wake na makato hayo kupelekwa katika mamlaka inayohusika na ikitokea ofisa huyo ana madeni zaidi ya moja, basi kiasi kinachoruhusiwa kukatwa kila mwezi kisizidi theluthi mbili ya

mshahara wa mwezi.

Vilevile, CAG Assad anabainisha makato yanayofanywa kwa baadhi ya watumishi yanakiuka Waraka wa Serikali wenye kumbukumbu namba C/CE.45/271/01/1/87 wa Machi 19, 2009, uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Anabainisha kuwa unawaelekeza maofisa masuuli wote kuhakikisha makato yote ya mishahara ya watumishi kwa ajili ya marejesho ya madeni katika mwezi yasizidi theluthi mbili ya mshahara wa mtumishi kwa mwezi.

INAENDELEA UK. 8

# Ajali Coaster, UDART zilivyoua Mwanza, Dar

**Na Waandishi Wetu**

AJALI mbili zilizotokea katika majiji ya Mwanza na Dar es Salaam zilizohusisha gari la Coaster na basi la Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (Udart), yamesababisha vifo vya watu wanne.

Katika ajali ya kwanza, watu watatu wamefariki dunia na wengine 48 kujeruhiwa vibaya baada ya gari aina ya Coaster iliyokuwa inatoka Igombe wilayani Ilemela kwenda jijini Mwanza kupata ajali baada ya kupasuka tairi la mbele.

Tairi hilo ni la upande wa kulia kisha kutumbukia kwenye mtaro wa maji katikati ya daraja la Kona ya Malaika jirani na Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

Ajali hiyo iliyotokea Alhamisi mchana, wakati dereva wa gari hilo namba T 454 AMQ alipojaribu kulipita lori la mchanga lililokuwa mbele kabla ya kugonga uzio wa daraja na kupasuka tairi na kutumbukia katika mtaro.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki, alisema walipokea majeruhi 48 na maiti mbili, ambapo 16 walitibiwa na kuruhusiwa.

Alieleza kuwa 18 hali zao zilikuwa mbaya, hivyo kuwahamishia katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando na wengine saba kubaki Sekou Toure.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya dharura na ajali, ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa Idara ya Dharura katika Hospitali ya Bugando, Dk. Erasto Sylivanus, alisema majeruhi waliowapokea ni 18, ambapo wanaume ni 10, wanawake 8. Wamo pia watoto wawili na kati ya hao watano walifanyiwa upasuaji.

INAENDELEA UK. 8




# Canada na Italia kuvutia uwekezaji Tanzania

**Na Grace Semfuko,** MAELEZO

NCHI za Canada na Italia zimekubaliana na Serikali ya Tanzania kuimarisha na kuvutia wawekezaji wa nchi hizo kuja kuwekeza nchini.

Katika vikao vya pamoja na mabalozi wa nchi hizo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Agellah Kairuki, mabalozi hao walisema watahakikisha wawekezaji binafsi wa nchi hizo wanakuja kuwekeza nchini hususan kwenye sekta za kilimo, dawa, utalii na viwanda.

Waziri Kairuki alisema hivi sasa Tanzania imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji na hivyo kuufanya uwekezaji kuwa rahisi na salama.

"Sisi Serikali ya Tanzania tumeweka mazingira mazuri, tunatarajia uwekezaji mkubwa kutoka kwa raia wa nchi hizi, tunawaomba waje tu na mitaji yao itakuwa salama," alisema Waziri Kairuki.

Alisema pamoja na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji pia watawaunganisha na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ili kuungana kwa pamoja na hatimaye kuleta ufanisi wa kibiashara.

Balozi wa Canada nchini Tanzania, Pamela O'Donnel, alisema wawekezaji wengi binafsi wa Canada waliopo Tanzania ni wa sekta ya madini na wamekuwa wakifanya vizuri kwenye sekta hiyo na kuongeza kuwa wanahamasisha wawekezaji wengi zaidi wa kampuni ndogondogo za Canada kuunganisha ubia baina yao na wawekezaji wa Tanzania.

Naye Balozi wa Italia nchini Tanzania, Roberto Mengoni, alisema sekta ya hoteli ndio uwekezaji mkubwa uliofanywa na wawekezaji wa Kiitalia nchini Tanzania na hivi sasa wanaangalia namna ya kuwekeza kwenye sekta ya dawa.

# Afungwa miaka 60 jela kwa kumbaka mtoto

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Wilaya na Mkoa wa Lindi, imemhukumu mkazi wa Kijiji cha Kilangara, Abubakari Kipande (58), kifungo cha jumla ya miaka 60 jela baada ya kupatikana na makosa mawili ya kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 11.

Hukumu hiyo ilitolewa na mahakimu wawili tofauti, James Karyhemaa na Franco Kiswaga, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka katika kesi mbili namba 106 na 107/2018, zilizofunguliwa.

Mshtakiwa Kipande alifunguliwa kesi hizo na mlalamikaji ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hizo, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuomba asipewe adhabu kali kwa kile alichodai ana familia akiwamo mke, watoto pamoja na wazazi wanaomtegemea, ombi ambalo lilitupiliwa mbali.

Baada ya utetezi huo, wanasheria wa serikali Abdurahamani Mohamedi Mshamu na Yahaya Gumbo, kila mmoja kwa wakati wake waliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye tabia kama hiyo.

Wakitoa hukumu katika kesi hizo, mahakimu hao, Karymaha na Kiswaga kupitia vifungu vya sheria 130 (1),(2) (e) na 131 (1) na (e) kanuni ya adhabu ya makosa sura 16 ya marejeo 2002, kwa nyakati tofauti, walipinga utetezi wake na kumhukumu kifungo cha miaka 30, katika kila kosa na kufanya aende gerezani kutumikia adhabu ya jumla ya miaka 60.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na wanasheria wa serikali Mshamu na Gumbo kuwa mshtakiwa Kipande, Februari na Agosti 13, mwaka jana, alimbaka mtoto huyo (jina linahifadhiwa) mwanafunzi wa darasa la pili.

Aidha, walidai mshtakiwa kwa mara ya pili alikamatwa na wanafunzi, wakati akifamfanyia kitendo hicho cha kinyama mlalamikaji, alipokuwa ameenda kichakani kujisaidia haja ndogo.

Wanasheria hao walisema wanafunzi hao walimfikisha mshtakiwa kwa walimu wao, ambao nao walimfikisha polisi kwa hatua kisheria.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakijipatia riziki kwa kuwaosha miguu watu waliotoka katika Soko la Mabibo maarufu kama Mahakama ya Ndizi jana. Soko hilo limejaa matope mengi yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha. Gharama ya kuosha inaanzia 200/- hadi 500/-. **PICHA: JOHN BADI**

# Mradi wa maji wa bil.17/- waja kunufaisha wananchi 400,000

**Na Rose Jacob, MWANZA**

ZAIDI ya shilingi bilioni 17 zimetolewa na serikali ya kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Kata ya Butimba hadi Igoma jijini Mwanza, ambako wananchi wa maeneo hayo wanakabiliwa na changamoto ya ukosekanaji wa maji.

Akizungumza katika utiaji wa saini ya mkataba wa ujenzi wa mradi huo baina ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Mwanza (MWAUWASA), mkandarasi China Civil Engineerring Consutruction Cooperatin (CCECC) na mhandisi mshauri kutoka Ufaransa, Mkurugenzi Mtendaji wa Mwauwasa, Mhandisi Anthony Sanga, alisema:

"Ujenzi huo ni utekelezaji wa programu ya uboreshaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya ukanda wa Ziwa Victria, utagharimu jumla ya shilingi bilioni 17.89 ambazo zimetolewa na serikali ya Tanzania kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)."

Aidha, Sanga alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha wananchi 400,000 ambao ni wakazi wa Jiji la Mwanza, hususan ukanda wa kusini watapata huduma ya maji kupitia bomba kuu la kusafirishia maji kutoka chanzo kipya cha Butimba hadi tangi la Igoma kupitia eneo la Sahwa.

Mradi huo unatarajia kukamilika kwa kipindi cha miezi 24 ikiwapo ni ujenzi wa kituo cha kusukumia maji, ujenzi wa tangi la chini ya ardhi la kuhifadhia maji lenye ukubwa wa lita 2,000,000 katika eneo la Sahwa.

"Eneo hilo la Sahwa ndio litakuwa kitovu cha kusambaza maji katika maeneo ya Buhongwa, Usagara na Kisesa, ujenzi wa tangi lenye ukubwa wa lita 2,000,000 kwa ajili ya usambazaji wa maji kwa wakazi wa ukanda wa kati na chini katika maeneo ya Nyashana, Mabatini na Nyakato," alisema Sanga.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Philis Nyimbi, ambaye alishuhudia utiaji saini huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwataka makandarasi ambao watajenga mradi huo kuhakikisha wanaujenga kwa kiwango cha juu bila kuwapo ujanja ujanja.

"Mkandarasi na mshauri hakikisheni mnajenga mradi huu kwa umakini ikiwamo kuhakikisha unakuwa na tija katika miundombinu... hii matakuwa mesaidia sana wananchi wetu na vizazi vijavyo viukute," alisema Nyimbi.

Aidha, Nyimbi aliwataka wananchi kuacha suala la kukwamisha mradi huo kwa kuiba vifaa na kuharibu miundombinu na kuondoa hofu juu ya upataji wa fidia, kwa kuwa watalipwa fidia wanayostahili.

# Asasi yawezesha wakulima bil. 712/-

**Na Gwamaka Alipipi**

ASASI ya kusaidia sekta binafsi ya kilimo nchini (PASS), imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 712 kwa wajasiriamali wa kilimo 929,172, kuanzia mwaka 2000 hadi 2018.

Wanufaika hao ni kutoka sekta mbalimbali za mifugo, uzalishaji wa mazao, usindikaji, biashara ya mazao, vifaa vya kilimo, umwagiliaji, ufugaji wa nyuki na samaki, pamoja na biashara ya pembejeo.

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS, Nicomed Bohay, aliyesema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu matokeo ya utendaji kazi kwa taasisi hiyo.

"Kwa namna tunavyofanya kazi katika kuunga mkono maeneo muhimu ya vipaumbele vya serikali hususani katika kutengeneza ajira na uwekezaji nchini, tumewawezesha wakulima wadogo kupata huduma za kifedha," alisema Bohay.

Alisema mwaka 2018 walinufaisha biashara 196,873 zilizojihusisha na mazao na huduma kwenye kilimo kupitia udhamini wa mikopo na huduma za maendeleo ya biashara katika mikoa 26.

Alisema mikopo hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha na kupanua wigo wa biashara za mazao na huduma katika kilimo nchini.

Aliongeza kuwa kwa mwaka huo huo pia walidhamini mipango ya biashara 15,564 yenye thamani ya Sh.bilioni 191 ambayo iliwasilishwa kwenye benki mbalimbali kwa ajili ya kuipatia fedha.

Alisema hali hiyo ni hatua kubwa ikilinganishwa na mipango ya biashara 623 yenye thamani ya Sh. bilioni 122.7 iliyowasilishwa mwaka 2017.

Alisema wastani wa fursa za ajira 387,804 zilitengenezwa katika sekta ya kilimo hapa nchini, ambapo wakulima wengi waliweza kuajiri wafanyakazi wa kuwasaidia katika uzalishaji.

"Vijana wamewekwa katika mazingira malumu wakijifunza masuala ya biashara katika kilimo cha mbogamboga pamoja na mifugo, kazi hiyo ilifanywa na kituo kinachosimamiwa na PASS kiitwacho Kituo cha ubunifu katika kilimo," alisema Bohay.



Baadhi ya vijana wa Kikosi cha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), wakiendelea na ujenzi wa nyumba za askari Magereza, Ukonga, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Bil. 1.5/- kuanzisha utalii wa faru weusi

**Na Novatus Makunga,** SAME

HIFADHI ya Taifa ya Mkomazi itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kuanzisha utalii wa faru weusi utakaokuwa wa kwanza hapa nchini na wa pili duniani, ambao utawawezesha watalii kuwaona kwa karibu wanyamapori hao waliopo hatarini kutoweka.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Abel Mtui, alisema kuwa aina hiyo mpya ya utalii wa faru inapatikana pekee nchini Afrika Kusini.

Mtui alisema Hifadhi ya Mkomazi inakamilisha kazi ya kuzungushia uzio wa umeme katika eneo la kilomita za mraba 13,000 ambalo ndilo litakalotumika kwa utalii huo unaotarajia kuanza rasmi mwezi Julai, mwaka huu.

Alisema utalii huo ni tofauti na mradi wa kukuza na kuzalisha faru weusi uliopo ndani ya hifadhi hiyo tangu mwanzoni mwa miaka ya 90 na ambapo ulianzishwa kwa ajili ya kuwaokoa wanyamapori hao waliokuwa hatarini kutoweka.

Akifafanua Mtua alisema kutokana na kushamiri kwa vitendo vya ujangili mwanzoni mwa miaka ya 80, faru weusi walihamishiwa Afrika Kusini na wengine nchi za Ulaya kama Jamhuri ya Czech na baadaye walianza kurudishwa na kuhifadhiwa katika mradi huo wa kuzalisha na kukuza faru.

"Kwa kuona uhitaji wa watalii wa kuona faru, Shirika la Hifadhi za Taifa nchini, Tanapa linaanzisha utalii wa faru katika mfumo wa aina yake ndani ya eneo maalumu la kutosha ambalo lina kila kitu kinachohitajika kwa faru," alifafanua.

Alisema kazi inayofanyika kwa sasa ni pamoja na kujenga miondombinu ndani ya eneo hilo zikiwamo barabara za kupita watalii, mabwawa ya maji kwa ajili ya wanyamapori hao pamoja na kufunga vifaa vya kisasa vya ulinzi na teknolojia ya kuwafuatilia faru.

Mwikolojia wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Glory Sumai, alisema faru weusi ni miongoni mwa wanyamapori wanaopatikana nchini ambao wamewekwa katika orodha ya waliopo hatarini kutoweka duniani na Shirika la Kimataifa la Muungano wa Uhifadhi (IUCN).

Aliwataja wanyamapori wengine ni mbwa mwitu na katika hifadhi hiyo pia wameanzishiwa mradi wa kuwazalisha na kuwakuza kwa ajili ya kuwasambaza katika mbuga nyingine za wanyamapori.

"Kuanzia mwezi wa saba watalii watakaoingia katika hifadhii hii wataweza kuangalia faru baada ya muda mrefu kuwa na mradi wa kuzalisha faru ambao ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha wanyama hao hawatoweki katika sura ya dunia," alisema.

Alisema kutokana na utafiti uliofanywa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori nchini (Tawiri), kuanzishwa kwa utalii huo wa faru kutawezesha idadi yao kuongezeka zaidi.

Alisema kuwa wanategemea watalii watakuwa wengi kwa kuwa hakuna mbuga nyingine ya wanyamapori ambayo mtu anaweza kuwaona faru kwa uhakika hapa nchini na nje ya Tanzania.

Akizungumzia mbwa mwitu Sumai alisema idadi yao imeongezeka kwa kuwa hivi karibuni waliingiza katika ikolojia ya Mkomazi na Tsavo Magharibi nchini Kenya zaidi ya mbwa mwitu 200.

# Waziri ampa mkandarasi maji siku 7

**Na Happy Severine,** MASWA

WAZIRI wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, amemtaka mkandarasi wa Kampuni ya Pett Cooperation anayejenga chujio la mradi wa maji Zanzui, lililoko wilayani Maswa, mkoani Simiyu, kukamilisha na kukabidhi mradi huo ndani ya siku saba tofauti na hapo atafukuzwa kazi na kufunguliwa mashtaka.

Akizungumza jana baada ya kukagua ujenzi huo majira ya saa 1:30 usiku, Waziri Mbarawa alisema hajaridhishwa na kasi ya ujenzi wa chujio hilo kwa sababu niwa siku nyingi na wenye kusuasua.

Alisema ni miaka minne sasa tangu uanze kujengwa mwaka 2015, wakati huo mkataba unaonyesha ulitakiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi tisa.

"Hii haikubaliki, wananchi wa hapa wanaugua magonjwa ya matumbo kwa sababu ya kunywa maji yasiyosafishwa...ikitokea kipundupindu athari yake ni kubwa na wananchi hawa wanataka wapate majisafi na salama kama eneo jingine la nchi yetu," alisema Waziri Mbarawa na kuongeza:

...lakini wewe, wewe kwa uzembe wako, kwa ukatili wako na kwa kutopenda nchi yetu umesababisha hili tatizo, una miradi zaidi ya 15 unayotekeleza hapa nchini na umekuwa ukipewa miradi huku na kule na kupeleka fedha kidogo pamoja na kuhonga ili upewe miradi, itakuwaje mtu mmoja upewe miradi mingi," alihoji.

Alimtaka Mkuu wa Kituo cha Polisi Maswa (OCD) kumweka mahabusu kwa saa mbili na baada ya hapo aandike maelezo vizuri ili kuhakikisha ifikapo Aprili 25, wananchi wa eneo hilo wanapata maji, huku akisisitiza kuwa ameshatoa fedha Sh. milioni 152.23 kwa ajili ya malipo yake na asipofanya hivyo atafungwa jela zaidi ya miaka miwili kwa kufanya utapeli wa miradi.

Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Dk. Seif Shekalaghe, alisema kwa sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 92 pamoja na matamko ya viongozi mbalimbali, mkandarasi amekuwa akisuasua kukamilisha mradi huo. Awali Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Maswa (Mwauwasa), Archades Anaclet, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2015, licha ya mradi kukabiliwa na changamoto ya malipo, lakini aliongezewa muda wa utekelezaji.

Aliongeza kuwa mkandarasi aliwahakikishia angekamilisha shughuli zote mwezi Desemba, mwaka jana na kukabidhi mradi, lakini hadi leo hajakamilisha, huku akiendelea kuwahakikishia atakabidhi mradi huo Aprili 30, mwaka huu.

Kwa upande wake mkandarasi wa mradi huo ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Pett Cooperation, Tryphone Elias, alisema changamoto za kucheleweshewa hati za malipo zimesababisha kuongezewa muda wa ujenzi, hali iliyofanya kupanda kwa bei ya bidhaa zinazotakiwa katika mradi huo.

Mradi umelenga kunufaisha wakazi zaidi ya 17,000.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Nidhamu iimarishwe Ligi Kuu Bara ikielekea ukingoni

**MSIMU** wa Ligi Kuu 2019/ 2020, ambayo ndiyo ligi ya juu kwa upande wa Tanzania Bara kwa sasa iko katika hatua za lala salama au tunaweza kusema inaelekea ukingoni.

Ligi hiyo tayari imeshaingia katika raundi ya 33, ikiwa na maana kuwa kwa timu ambazo hazina viporo, zitakuwa zimebakisha michezo mitano ili kumaliza msimu.

Hata hivyo, msimu huu umekuwa na idadi kubwa ya mechi za viporo, ambazo zilitokana na Simba kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Licha ya ligi hiyo kukosa mdhamini mkuu, na inayoshirikisha timu 20 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, ndiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara wanaokwenda katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ikiwa imefika hatua za lala salama, wasimamizi wa ligi hiyo ambao ni Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanatakiwa kuongeza umakini katika viwanja vyote vinavyotumika.

Usalama huo unatakiwa kuwekwa kuanzia kwa wachezaji, waamuzi, mashabiki na viongozi wote ambao wanafika uwanjani kushuhudia mechi hizo zinazoendelea, huku kila timu ikiwa na malengo.

Kama suala la usalama litakuwa dogo katika mechi hizo, hali ya hatari inaweza kutokea na kusababisha michezo kuvunjika badala ya kuchezwa kwa dakika 90 kama ilivyotarajiwa.

Viongozi wa TFF katika mikoa inayopokea timu za Ligi Kuu wanatakiwa kujipanga imara kuhakikisha mechi zote zinamalizika kwa amani na wahusika wote kuondoka wakiwa salama na kusahau suala la kugawa pointi za mezani.

Wakati viongozi hao wakitimiza majukumu yao, wachezaji nao wanatakiwa kuwa na nidhamu kwa kuwaheshimu waamuzi na kuacha kujichukulia sheria mkononi, jambo ambalo linaweza kuwaweka katika mazingira ya hatari.

Mchezaji kufungiwa kwa sababu ya kosa la utovu wa nidhamu ni suala linaloweza kumaliza kipaji chako, huku ukiiweka katika mazingira magumu familia yako ambayo ilikuwa inakutegemea.

Mbali na wachezaji, waamuzi pia wanatakiwa kufuata vema sheria 17 za mchezo huo na hapo, gazeti hili linaamini kwamba vurugu na ngumi zinazorushwa zitabakia kuwa historia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nipashe bila kusahau linawakumbusha mashabiki na wanachama wa timu hizo zinazoshiriki Ligi Kuu kuwa watulivu na kuonyesha nidhamu katika kipindi chote wakati mechi zinachezwa.

Nimelazimika kuandika maoni haya, kwa lengo la kukumbushana kuimarisha nidhamu baada ya shabiki mmoja wa Yanga kuonekana akienda kumsukuma mwamuzi namba moja baada ya kutokubaliana na uamuzi wake wakati wa mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar uliochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, Morogoro Jumatano iliyopita.

Nidhamu hiyo pia itapendeza ikionekana kabla na baada ya mechi kumalizika, kwa sababu itasaidia kuwajenga wachezaji kujitambua na kupambana kusaka matokeo chanya ili kuwafurahisha mashabiki wao na vilevile kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa au kutoshuka daraja.

Nidhamu ikiimarishwa, bingwa bora atapatikana na nchi itapata mwakilishi mwenye uwezo kwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Watanzania tunajiangusha wenyewe!

**'LAHAULA!** (neno linalodhihirisha mshangao au sikitiko; tamko linalotumiwa na mtu anapotanabahi baada ya kusahau au kushtukia jambo). Ndivyo Simba na Yanga zilivyotuharibu hata kutokuwa na mapenzi na timu zetu za taifa!

Simba na Yanga zikutanapo, watu huanza kuingia uwanjani takribani saa nne asubuhi. Kwa hali hiyo uwanja hujaa na kusababisha watazamaji wengi kukosa nafasi, hivyo kubakia nje ya uwanja au kurudi nyumbani. Wengi wetu twashindwa kutambua kuwa wakati timu za taifa zinapocheza na timu za nje, wingi wetu uwanjani ni kama 'mchezaji wa 12' yaani zaidi ya wachezaji 11 wa kawaida.

Tunapowapa wachezaji wetu hamasa (hamu na shauku ya kufanya jambo; changamoto, shime, mdadi) hupata nguvu ya kucheza kwa bidii zaidi ili kupata ushindi na kuwafurahisha watazamaji na Watanzania kwa jumla. Ndivyo wafanyavyo wenzetu huko ughaibuni (nchi zilizoko mbali na Tanzania).

Tatizo letu ni kutekwa mno na ushabiki (hali au tabia ya kupenda sana jambo au kitu fulani, hali ya kuwa shabiki, tendo la kushabikia) wa Simba na Yanga kuliko timu za Taifa. Timu zetu za Taifa zinapopambana na timu ngeni, idadi ya watazamaji wanaofika uwanjani ni ndogo mno hata kuwashangaza wageni! Tena baadhi ya watazamaji wetu huingiza u-Simba na u-Yanga kwa kuwazomea wachezaji wa Simba na Yanga wanapopigwa chenga na wageni!

Ingawa yalifanywa matangazo mengi kwenye magazeti, redio na runinga kuwahamasisha Watanzania kwenda uwanjani kwa wingi ili kuipa hamasa timu yetu ya Serengeti Boys, waliokwenda uwanjani hawakujaza hata robo ya uwanja! Matokeo yake vijana wetu wakafungwa mabao 5-4 na wenzao wa Nigeria.

Mechi ya pili pia uwanja haukujaa watazamaji wakati Serengeti Boys ilipopambana na Uganda ingawa watu walitangaziwa kuingia uwanjani bure kwani ilipoteza mchezo kwa kufungwa mabao 3-0. Inatoa picha gani timu zetu kufungwa kila mara na timu ngeni kwenye uwanja wetu?

Kwa hali hii, timu ngeni hudhani Watanzania hatupendi mchezo wa kandanda ndio maana hatuendi uwanjani kuzishangilia timu zetu. Jambo hili huzitia hamasa timu ngeni kucheza kwa bidii na kupata ushindi. Ina maana Simba na Yanga ni bora kuliko timu za taifa? Mbona twajidhalilisha na kujiaibisha mbele ya wageni? Aibu iliyoje!

Twapaswa kutambua kuwa tunapozibeza (kitendo cha kupuuza kitu, mtu au jambo; kitendo cha kuonyesha hisia za kejeli kwa mtu) timu zetu za taifa tunajidhalilisha wenyewe na kuonekana kama mazezeta yaani watu tuliorukwa na akili.

Hata timu zinazokuja kupambana na Simba au Yanga, hujua uhasama wa timu hizo ulivyo. Ndo maana huja na jezi zao ili kuziuza au kuzigawa bure kwa timu mojawapo.

Ndio maana wahenga walisema "Ujinga wa kuuza si ubaradhuli wa kununua." Ubaradhuli ni upumbavu. Maana yake ni heri kuwa mjinga wa kuuza kuliko kuwa mjinga wa kununua. Hutumiwa kuwakumbusha watu umuhimu wa kuwa makini na kuwa tahadhari wakinunuapo au wanapopendekezewa kitu fulani.

Huenda baadhi ya watazamaji hukataa kwenda viwanjani wakati timu za taifa zinapocheza kwa hofu ya kufungwa na kujutia fedha walizotoa kununua tiketi. Ifahamike kuwa idadi ndogo ya wananchi wanaokuwa viwanjani huweza kuwa sababu ya timu zetu za taifa kushindwa na wageni.

Timu zinapoingia uwanjani na wachezaji wetu kuona idadi ndogo ya watazamaji, hukata tamaa, na kutawaliwa na wasiwasi wa kushindwa. Matokeo yake huwa mabaya na kuwafanya wananchi kutokuwa na uhakika wa ushindi timu zetu zinapopambana na timu ngeni.

Twapaswa kutambua kuwa kandanda ni mchezo wa bahati kwa kuwa kuna kukosa na kupata.

Kama timu mahiri duniani hupoteza mechi nyumbani zinapopamba na timu ngeni, sembuse timu za Tanzania? Wakati mwingine wingi wa watazamaji viwanjani huweza kuwa sababu ya timu kupata ushindi kutokana na kushangiliwa kwa bidii na timu ngeni kuzomewa mara kwa mara zinapopoteza mpira au kushindwa kufunga.

Watanzania twapaswa kuzithamini timu zetu za vilabu na taifa zinapopambana na timu ngeni. Tuachane na ujinga wa kuzishabikia timu ngeni badala ya timu zetu za vilabu na taifa. Tuondokane na ubereuzaji yaani hali ya mtu kujifanya kuwa hana habari ya jambo kwa sababu hataki kushiriki katika utendaji wake. Hii ni aina fulani ya ujuha yaani upumbavu.

Timu zetu za vilabu na taifa zinaposhinda michezo ya kimataifa, Tanzania hujulikana zaidi kama zilivyo Nigeria, Ghana, Misri, Algeria, Cameroon na Ivory Coast kwa uchache. Itapendeza kama Tanzania nayo itaingia kwenye orodha ya nchi zenye timu zinazoogopwa hata kwa kutaja tu majina yao.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# HABARI PICHANI



Rais Dk. John Magufuli akiwa pamoja na waumini wengine akishiriki Misa Takatifu ya Alhamisi Kuu katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Petro Parokia ya Oysterbay, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kiluther Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Amoni Kinyunyu (kushoto), akisalimiana na Askofu mstaafu wa Dayosisi hiyo, Askofu Peter Mwamasika, nje ya Kanisa Kuu Usharika wa Dodoma, baada ya Ibada ya Ijumaa Kuu iliyofanyika kanisani hapo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya wazazi wakinunua viatu kwa ajili ya watoto wao, katika Mtaa wa One Way jijini Dodoma jana, ikiwa ni maandalizi ya sikukuu ya Pasaka inayotarajiwa kusherehekewa kesho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma, wakifanya maandalizi ya sikukuu kwa kununua kuku, katika Soko Kuu la Majengo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Sehemu ya waumini wa kikristo waliohudhuria ibada ya Ijumaa Kuu katika kanisa la KKKT Azania Front, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Sehemu ya umati wa waumini wa kikristo waliohudhuria ibada ya Ijumaa Kuu katika kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph, Barabara ya Sokoine, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CAG Assad anusa uonevu wa makato

INATOKA UK. 3

"Kinyume cha matakwa ya sheria na waraka nilioutaja hapo juu, nimebaini mishahara ya watumishi 229 imekatwa juu ya theluthi moja," Prof. Assad anabainisha.

Anasema makato hayo yameshuhudiwa katika taasisi saba zilizokaguliwa ambazo Wizara ya Fedha na Mipango, watumishi 21 na Sekretarieti za Mkoa ya Geita 30, Mwanza 18, Tanga 39, Mbeya 21, Katavi 16 na Kilimanjaro 84.

"Katika hali hii, watumishi ambao wanapokea kipato kidogo tofauti na matarajio, wataanza kutafuta njia mbadala za kuongeza kipato ikiwamo ubadhirifu wa muda ama mali za taasisi na kupoteza uwezo katika kujikita na kazi zao hivyo, kupelekea kutotekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

"Kama ilivyokuwa katika taarifa yangu iliyopita, mwaka huu pia kuna mwendelezo wa kutozingatia sheria hii. "Ulinganisho nilioufanya katika taarifa hii na ile iliyopita inaonyesha udhibiti katika kuzuia watumishi wasikope zaidi unaendelea kushuka kwa kuwa mwaka wa fedha 2016/2017, kulikuwa na taasisi 12 zenye watumishi 278, wakati mwaka huu taasisi saba zilizopitiwa zina watumishi 229, wanakatwa kiwango kikubwa kutokana na mikopo iliyokopwa katika taasisi mbalimbali na hivyo kusababisha kupokea mshahara chini ya theluthi mbili kwa mwezi.

"Katika hali hii bado naendelea kusisitiza katika ushauri nilioutoa maofisa masuuli kuongeza udhibiti kwa watumishi kutokuwa na mikopo mingi na mikubwa kwa kutokopa hadi itakapopitiwa na kuthibitishwa kuwa mkopo wa awali umeisha au hautavuka kiwango cha juu cha makato," CAG Assad anashauri.

Mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu pia anapendekeza maofisa hao kuwasiliana na wakopeshaji ili wasitoe mikopo kwa watumishi ambao makato yatasababisha kupokea mshahara chini ya theluthi moja ya mshahara wa mwezi na ikitokea wamekopa pasipo taasisi kujua, basi inashauriwa wakopeshaji hao wasilipwe kupitia mshahara.

"Halikadhalika, mfumo wa Lawson utumike kama njia ya kudhibiti ukopaji holela," alisema.

Lawson ni mfumo unaotumiwa na serikali katika malipo na ajira za watumishi wa umma.

Wakati wa Bunge la Bajeti mwaka jana, baadhi ya wabunge walieleza bungeni kuhusu kadhia ya watumishi kukatwa kiwango kikubwa kwenye mishahara yao kurejesha mikopo, wakieleza kuwa waathirika wakubwa wa mikopo hiyo ni walimu.

Wabunge hao pia walibainisha kuwa marekebisho ya sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), yaliyoongeza kiwango cha makato kutoka asilimia nane hadi 15 ya mshahara wa mnufaika wa mkopo wa bodi hiyo.



Mchuuzi wa madafu akimhudumia mteja wake katika Mtaa wa South, katikati ya Jiji la Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Makanisa yaonya njaa

INATOKA UK. 2

kuhubiri amani hii tuliyonayo ambayo Mungu ametupatia juu ya nchi yetu, hivyo kila Mtanzania anatakiwa kuilinda na kuienzi," alisema.

Aliwahimiza kuunga mkono juhudi za serikali katika uwajibikaji kwenye maeneo ya kazi ili kufikia uchumi wa kati.

Alisema serikali imekuwa ikisisitiza kuwajibika hivyo pamoja na kanisa kuwajibika kwenye maombi kwa ajili ya taifa lazima wafanyekazi tena kwa malengo.

Naye, Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Askofu Amon Kinyunyu, alitoa wito kwa jamii kuendelea kujenga moyo wa upendo pamoja na kuvumilia ili kuimarisha amani iliyopo.

"Tukio la kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo pale msalabani ni kwa ajili yetu sisi alijitoa ili kutukomboa sisi wanadamu," alisema.

Alisema tukio hilo linawakumbusha kuishi kwa umoja na upendo na kusameheana.

Aidha, alisema baada ya kifo hicho msalabani watu wote wamewekwa huru kwa hiyo hakuna haja ya kuendelea kujenga chuki.

Ibada hiyo pia ilihudhuriwa na Askofu mstaafu wa Dayosisi hiyo, Dk. Peter Mwamasika, aliyeomba watu kuendelea kuitunza amani na kuwaombea viongozi wote.

**Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi, (Arusha) na Peter Mkwavila na Ibrahim Joseph (Dodoma)**

# Askofu aonya viongozi wanaowaonea wanyonge

INATOKA UK. 2

ta ujumbe mfupi wa maneno kwenye simu unasema 'yule babu wa Sumbawanga au Tanga ameshafika, sema nikuunganishie upate mali'.

Ibada hiyo ambayo Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam Mwdhama Polycarp Kardinali Pengo, alikuwapo Padri Mbaula alisema ujumbe mfupi kwenye simu umesababisha mafarakano kwenye ndoa na jamii kwa ujumla.

"Wanaotuma meseji ni watoto wetu na wengine wanaotuma ni wazee ambao hawataki kuzeeka, leo hii Yesu analia sana na mapato ya siri na matumzi ya siri katika familia, tujifunze kupanga pamoja kile mlichopata," alisema.

Alisema wakati wa maadhimisho hayo ya kifo cha Yesu Kristo, analia simu ambazo ndio chanzo na mambo mengi ambayo hayampendezi Mungu.

Pia alisema kilio cha Yesu kipo katika ile mianzo midogo ya dhambi ambayo husababisha kuwa kubwa.

"Vyanzo vyake ni katika majivuno, viburi, kujiruhusu kutawaliwa na hasira, kuruhusu badala ya roho kuongoza mwili, mwili unaongoza roho kwenye dhambi ya mihemko," alisema.

Padri Mbaula amewataka waumini waziombee familia, taifa na viongozi ili wafike kwenye furaha na amani.

**UPENDO WA UNAFIKI**

Wakristo wametakiwa kuacha upendo wa kinafiki kama Yuda Eskarioti aliyemsaliti Yesu, badala yake wawe wa kweli kama dini inavyotaka.

Hayo yalisemwa jana na Paroko msaidizi Daud Mlemeta katika ibada ya Ijumaa kuu ilifanyika Kanisa Katoliki jimbo Kuu la Dodoma.

Alisema hakuna haja wakristo kutenda mambo maovu nje ya kanisa na wakienda ibadani wanajifanya watakatifu, kitu ambacho sio sahihi.

Alisema toba waliofanya kipindi cha Kwaresma basi waendelee nayo ili waweze kuuona ufalme wa mbinguni.

Alisema hakuna haja ya mkristo kuigiza maisha ya upendo, bali kinachotakiwa ni kuyatenda na kuyaishi.

**Imeandikwa na Mary Geofrey, Romana Mallya (Dar) na Renatha Msungu (Dodoma).**

## Ajali Coaster, UDART zilivyoua Mwanza, Dar

INATOKA UK. 3

"Majeruhi watano ambao walikuwa wamepata majeraha katika maeneo ya ubongo, tumbo na mfupa tuliwafanyia operesheni, lakini kati ya hao majeruhi mmoja mwanamke ambaye hajatambulika alifariki dunia wakati akiwa katika chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) kutokana na kuumia katika maeneo ya tumbo, sehemu za ubongo na mifupa," alisema Dk. Erasto.

Vilevile Erasto alisema, dereva wa gari hilo, Mwaka Isabuki yupo ICU kutokana na kuumia katika sehemu ya ubongo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Philis Nyimbi, akizungumza baada ya kuwatembelea majeruhi waliolazwa katika Hospitali za Sekou Toure na Bugando, alisema wamiliki wa magari wanapaswa kuyafanyia matengenezo mara kwa mara na kuhakikisha madereva wanafuata sheria ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Majeruhi waliohojiwa Ibrahimu Mtuly (Sekou Toure) na Dosele Mbute (Bugando) walisema, chanzo cha ajali ni tairi la upande wa kulia wa Coaster hiyo kupasuka, baada ya dereva kujaribu kulipita lori la mchanga.

Katika ajali ya pili, mtu mmoja anadaiwa kupoteza maisha kutokana na ajali iliyotokea eneo la Magomeni jijini Dar es Salaam iliyohusisha basi la Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka(Udart) maarufu kama Mwendokasi, lenye namba za usajili T 973 DGV na gari dogo aina ya Nissan March lenye namba T 968 DNZ.

Ajali hiyo ilitokea jana mchana eneo la Magomeni Mapipa jijini Dar es Salaam na kusababisha dereva wa gari ndogo kufariki dunia papo hapo.


Katika eneo la tukio basi hilo liliharibika vibaya upande wa kushoto wa mlango wa mbele wa dereva na kusababisha vioo vyote kuvunjika.

Gari ndogo iliharibika vibaya kwa kukatika vipande vipande, huku dereva aliyekuwa akiendesha gari hilo ambaye inadaiwa alifariki dunia papo hapo baada ya kujeruhiwa vibaya.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Kipolisi Ilala, Mussa Taibu, alikiri kutokea kwa ajali hiyo na kusema kuwa, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa ndiye mwenye jukumu la kutoa taarifa hiyo.

Nipashe lilimtafuta Kamanda Mambosasa kupitia simu yake ya mkononi ambayo hata hivyo, iliita bila majibu.

**Imeandikwa na Rose Jacob (Mwanza na Mary Geofrey (Dar).**



# Shirika lawezesha askari mafunzo ya hifadhi

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

SHIRIKA la Maendeleo ya Jamii la OIKOS, limegharamia asilimia 70 ya mafunzo yaliyotolewa kwa askari jamii (VGS ) katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Enduiment (EWMA).

Meneja wa jumuiya hiyo, Peter Millanga, alisema mafunzo hayo ya wiki tatu, yamegharimu Sh. milioni 20, lengo likiwa ni kuhakikisha wanawajengea uwezo na ukakamavu askari hao.

"Mafunzo haya yamefadhiliwa na shirika la OIKOS asilimia 70,Kinapa asilimia 20 na Shirika la Honey Guide Foundation asilimia 10, ili kuhakikisha wanalinda ipasavyo wanyama wetu," alisema Millanga.

Aliwataka askari waliopatiwa mafunzo hayo kufanya kazi kwa weledi na kudhibiti mianya ya rushwa, hususani kwa askari waliopo kwenye geti za kuingilia na kutokea hifadhini.

"Hakikisheni mnasimamia watu wanaopita katika mageti hayo kwa ajili ya utalii wanalipa kodi, fanyeni hivyo ili mapato yapatikane, msikubali kudanganywa na kupewa rushwa," alisema Millanga.

Mkurugenzi wa OIKOS, Silyvia Ceppe, aliwataka askari hao, kuhifadhi mazingira na kuyatunza, kutokana na hali ya sasa ya mabadiliko ya tabianchi.

Aliwataka askari hao wakawe mabalozi wa uhifadhi na hasa katika kipindi hiki ambacho ukame umeshika kasi, kwa baadhi ya maeneo nchini, hali itakayoongeza watu wengi kuharibu mazingira kwa kujitafutia kipato.

Alifafanua kuwa mazingira yataharibika kwa watu kukata miti, kuchoma mkaa pamoja na ujangili kutokana na kukosekana kwa mvua, hali ambayo itasababisha watu kukosa malisho na chakula.

Hata hivyo alisema shirika hilo limewekeza EWMA kwa kuwasaidia umeme wa jua (sola) ili kujiendesha pamoja na miradi ya kuwawezesha wanawake katika elimu ya ujasiriamali.

Pia alisema pamoja na uwekezaji huo, wametoa mabomu ya pilipili, baruti na tochi maalum 40 kwa wananchi ili watumie kufukuza wanyamapori wakali nyakati za kilimo wanapovamia maeneo ya wakulima.

Aliongeza kuwa wanatarajia kutoa mafunzo ya utengenezaji bidhaa kwa kutumia ngozi na wanategemea kuwekeza katika Kata ya Sinya, ambayo imeonekana kuwa na vivutio vya utalii.

"Hadi sasa tumeshatoa elimu ya ujasiriamali kwa wanawake 300 katika vikundi huko Sinya na sasa tupo Kata ya Kamwanga na Olmolog," alisema Silyvia.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, aliwataka kuwa mabalozi katika kupiga vita ujangili na biashara za magendo, ikiwamo utoroshwaji wa mifugo kwa njia za panya, kuelekea nchi jirani.

Alisema wilaya hiyo imejikita katika uhifadhi na ufugaji, lakini kipaumbele cha kwanza ni uhifadhi, kukiwa na uhifadhi mzuri hata mifugo itakuwa salama.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Yefred Myenzi, akisoma ajenda za kikao cha Baraza la Madiwani juzi. Kushoto ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jackson Sipitieck na Katibu Tawala wa Wilaya, Zuwena Omary. **PICHA: GIFT THADEY**

# Biteko afagilia ukuta kupaisha mapato tanzanite

**Na Allan Isack,** MIRERANI

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, amesema tangu kujengwa kwa ukuta wa kuzuia utoroshwaji wa madini ya tanzanite wilayani Simanjiro mkoani Manyara, serikali imeongeza mapato, kwa kukusanya kodi Sh. bilioni mbili kwa mwaka 2018/19.

Akizungumza na wachimbaji wadogo wa tanzanite, Biteko, alisema awali serikali ilikuwa ikikusanya kodi Sh. milioni 70, lakini baada ya kujengwa kwa ukuta huo, mapato yameongezeka hadi kufikia kiasi hicho.

Biteko aliiagiza wizara yake kuwaongeza wathaminishaji wa madini katika eneo hilo, kutokana na idadi kubwa ya watu wanaohudumiwa kwenye migodi hiyo, wamekuwa wakicheleweshewa huduma kutokana na uchache wa watumishi.

"Katibu Mkuu wa wizara nakuagiza ongeza wathaminishaji wa madini haraka, kwa sababu wachimbaji na wanafanyabiashara, wanaonunua madini, wamekuwa wakilalamika mizigo yao inapakiwa kwa wakati, lakini wanachelewesha kuitoa kwa wakati kutokana na kutokufanyiwa tathmini kwa haraka," alisema Biteko.

Aliwataka watumishi wa madini kuacha tabia ya kufunga ofisi hizo mara kwa mara, badala yake watumie muda mwingi kukaa ofisini kuwahudumia watu kwa sababu wanatumia nguvu nyingi kufikisha madini katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, aliwataka wachimbaji hao, kufuata sheria, kanuni na utaratibu uliowekwa wakati wakiingia ndani ya machimbo hayo.

# Wadau kilimo wasisitizwa vita ya mabadiliko tabianchi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WADAU wa kilimo na wakulima wa maharage, wametakiwa kushirikiana na serikali kupambana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa ili waweze kuzalisha mazao yenye tija.

Akizungumza jana wakati akifungua warsha ya siku mbili iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), kupitia mradi wa Afrika Mashariki wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa kwa Tanzania, Kenya na Uganda, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, aliwahimiza washiriki kushirikiana na serikali zao, ili kukabiliana na changamoto wanazopata.

Alisema mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa nchi zote duniani, zimepata athari na kusababisha shughuli za kiuchumi katika nyanja za mifugo na kilimo kuathirika.

"Kama sasa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara, tunapita katika kipindi ambacho hatujawahi kupitia, hakuna mvua mwezi huu, kitu ambacho sio cha kawaida kutokea, mazao yameoteshwa hayaoti kwa ukame, sasa lazima tujipange kukabiliana na hali hii na ili tufanikiwe lazima tushirikiane," alisema.

Alisema kupitia mradi uliotetwa na SNV, ni vema wakaweka mikakati kabambe ili wakulima na wadau wa zao hilo waweze kukabiliana na athari zinazojitokeza kwao. Kwitega alisema maharage muhimu kwa chakula, hivyo lazima kuweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wake kwenye wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa, unaosababisha ukosefu wa mvua za uhakika na kujitokeza kwa joto kali.

Msimamizi wa mradi huo, Godfrey Kabuka, alisema mradi huo upo katika nchi zaidi ya 15 za Afrika na duniani nchi zaidi ya 30 na umelenga kusaidia wakulima wadogo ili wajikwamue kimaisha, kwa kuwapatia mbinu za kukabiliana na mabadiliko yanayojitokeza. "Hapa tunawahimiza sana matumizi ya mbegu zilizo sahihi zinazotolewa na wataalamu wetu na kuepuka kutumia mbegu zilizotumika miaka ya nyuma au za kienyeji," alisema.

Alisema unatekelezwa kwa miaka mitano kwa gharama ya Euro milioni 39 zilizotolewa na SNV.

Warsha hiyo ilikutanisha wakulima wadogo wa maharage, wasambazaji wa pembejeo, watafiti wa kilimo, taasisi za fedha na wadau wengine wa kilimo kutoka nchi hizo tatu za Afrika Mashariki zinazotekelezwa mradi.

Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Uholanzi, Annamarie Groot, alisema mabadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa, yanahitaji nguvu ya pamoja kuyashughulikia na sio mmoja mmoja au nchi moja kwa faida ya kizazi kijacho.





# Ripoti yaibua yaliyojificha Mwanga

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

RIPOTI ya matokeo ya utafiti kuhusu tathmini ya thamani ya fedha kwenye shughuli mbalimbali zinazofanywa kwa kutumia rasilimali za umma ili kuongeza utawala bora na uwajibikaji hasa kwenye sekta ya maji katika Wilaya ya Mwanga, imeibua changamoto mbili kubwa ambazo ni ushiriki mdogo wa wananchi katika masuala ya maji na kukosekana kwa taarifa za mapato na matumizi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la kiraia la Kinshai, linalotekeleza mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS), Veronika Shao, amesema matokeo ya utafiti huo yanatokana na taarifa zilizokusanywa katika kata 10 za wilaya hiyo.

"Ripoti hii ni matokeo ya taarifa zilizokusanywa kutoka kata 10 za Wilaya ya Mwanga kuanzia mwezi Februari hadi Machi, mwaka huu. Kutokana na matokeo, changamoto mbalimbali zinazowakabili wanajamii kuhusu utumiaji, upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za maji ziliibuliwa.

"Kuna kukosekana ama ushiriki mdogo wa jamii kuhusu masuala yahusuyo maji, kukosekana kwa taarifa za mapato na matumizi ya rasilimali za maji kwa baadhi ya vijiji na kata kwa sababu zilizo juu ya uwezo wa jamii kuzielewa, mwamko mdogo wa jamii katika uchangiaji gharama za maji na uhaba wa maji unaosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi na mgao wa maji usio mzuri," alisema.

Mradi huo unatekelezwa na Kinshai kwa ufadhili wa Shirika la The Foundation for Civil Society.

Aidha, wakati anasoma ripoti hiyo, Mhadhiri wa Kitivo cha Jamii na Maendeleo Vijijini wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prosper Kimaro, alisema utafiti huo ulifanywa katika kata za Mgagao, Lembeni, Kileo, Jipe, Lang'ata, Shighatini, Kighare, Msangeni, Mwanga na Kirya.

Alisema kuwa idadi ya washiriki wote katika utafiti huo walikuwa 365 ambao ni wanaume na wanawake.

Awali, mtaalamu mwelekezi kuhusu dhana ya ufuatiliaji wa rasilimali za umma na mchakato wa bajeti, Gamaliel Mbalase, aliwaeleza wananchi hao wa Wilaya ya Mwanga kuwa ufuatiliaji huo unaongeza ushiriki wa wanajamii katika ufuatiliaji wa rasilimali fedha na mchakato wa bajeti na utekelezaji wake.

Zaidi alifafanua, kwamba PETS ni chombo kinachotumika katika kufuatilia au kuchunguza jinsi rasilimali za umma zinavyotumika kutoka kwenye ngazi zote za kiserikali na kisekta.

Kwa upande wake, Mhandisi wa Maji wa Sektretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Victor Nassari, alionya kuhusu vitendo vinavyoendelea vya uharibifu wa vyanzo vya maji na baadhi ya wananchi wa kata kadhaa kugoma kufungiwa dira za maji, wakidai maji hayo hawawezi kulipia kwa sababu ni vyanzo vya asili vilivyopo katika maeneo yao.

"Shida kubwa iliyopo Wilaya ya Mwanga, wananchi baadhi yenu hamtaki kufungiwa dira za maji na kwa hasira mnakwenda kuziharibu zile zilizofungwa tayari. Tutachukua hatua kwa atakayebainika kuanzia sasa," alisisitiza Nassari.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, akizungumza na wadau hao na kamati za maji kutoka kata 10 za wilaya hiyo, alisema serikali itapambana kwa kila namna kuhakikisha katika miradi ya maji inayotekelezwa hakuna matumizi mabaya ya fedha wala ya madaraka.

"Tuna vyanzo vingi vya maji katika Kata ya Kileo na Shigatini, lakini hatujaweza kuvitumia ipasavyo. Tumesema katika miradi tuliyonayo hivi sasa tunahakikisha wananchi wanapata maji wakati wote, lakini mapato yake na miundombinu yake inafanana na thamani ya fedha ama zinazokusanywa na kamati za maji au gharama za ujenzi," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, Thomas Apson (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua ripoti ya utafiti wa mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS), katika sekta ya maji wilayani humo juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Bakwata yatoa siku 30 kusajiliwa ndoa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BARAZA Kuu la Waislamu Mkoa wa Kilimanjaro (Bakwata), limetoa siku 30 kwa viongozi wake wa madrasa, misikiti na waliopewa dhamana ya kufungisha ndoa kwa mujibu wa sheria, kutekeleza agizo la Mufti wa Tanzania, Shekhe Abubakar Zuberi aliyetaka wasajiliwe.

Muda huo maalum wa kutekeleza agizo hilo, ulitangazwa jana na Katibu wa Bakwata mkoani hapa, Awadh Lema, wakati akizungumza na viongozi mbali mbali wa misikiti wakiwamo maimamu wa mkoa huo.

Aprili 13, mwaka huu, Bakwata, ilizindua mpango mpya wa vyeti vya ndoa, usajili wa madrasa na walimu, misikiti na utoaji wa vitambulisho kwa wafungishaji ndoa katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Kiislamu ya Al-Haramain, iliyopo Kariakoo, Ilala, jijini Dar es Salaam.

"Nimetoa siku 30 kwa Mkoa wa Kilimanjaro ili wahusika waweze kujisajili kulingana na maelekezo ya Mufti na endapo mtu hatajisajili, Bakwata itashindwa kumtambua na atakuwa siyo mtu sahihi kutekeleza majukumu hayo," alisema Lema.

Alisema kusajiliwa kwa misikiti na madrasa kutasaidia kuyaweka mambo wazi pamoja na kuhifadhi kumbukumbu zao katika ofisi za baraza hilo katika ngazi mbalimbali. Kwa mujibu wa Lema, kuna umuhimu mkubwa kwa madrasa na misikiti yote kujulikana na kwamba utambulisho huo utaisaidia Bakwata kusaidiwa katika mambo mbalimbali.

Hata hivyo, Kaimu Shekhe wa Mkoa wa Kilimanjaro, Shaaban Mlewa, wakati anazungumza na viongozi hao kuhusu vyeti vya ndoa, aliwataka wote wenye vitabu vya ndoa vya zamani kuviwasilisha ofisini kwake mara moja na kuchukua vipya.

Kutokana na utekelezaji wa agizo hilo, Imamu wa Kijiji cha Sanya Juu, Wilaya ya Siha, Hamza Shekhe na Mwenyekiti wa Bakwata Wilaya ya Hai, Omari Maamud kwa nyakati tofauti wameeleza kuwa mpango huo ni mzuri na utasaidia kufahamu mambo mbalimbali yanayofanyika katika madrasa zao na misikiti yao.

## Vitambulisho vya machinga vyamtoa ofisini

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

ZOEZI la ugawaji wa vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga ambavyo vimechapishwa na Rais Dk. John Magufuli, kwa ajili ya kuwasaidia wasibughudhiwe wanapofanya biashara zao, limemsukuma Mkurugenzi mpya wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigara, kutokaa ofisini.

Mkurugenzi huyo ameanza kazi ya kufanya ukaguzi wa ugawaji wa vitambulisho hivyo vya wajasiriamali wadogo, ikiwa ni siku chache baada ya kuripoti kazini, akitaka kupata uhalisia wa zoezi zima linavyoendelea.

Jana, Msigara alilazimika kutoingia ofisini na kwenda moja kwa moja katika Kata ya Mabogini kuongea na watumishi wa kata, kusikiliza kero za watumishi na wananchi wa eneo husika.

"Nimesema sikuja kushinda ofisini tu, nimekuja kufanya kazi na kazi yangu ya kwanza naanza nayo ni kufuatilia utekelezaji wa agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dk. John Pombe Magufuli ili kupata uhalisia wa zoezi zima," alisema.

Akizungumza na watumishi hao, Msigara alisema lengo la ziara hiyo pia ni pamoja na kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya kata husika kwa kufuatilia, kusimamia, kuhakikisha kuna kuwapo na matumizi bora ya fedha za umma pamoja na kufanya ukaguzi wa zoezi la ugawaji wa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo. Katika mkutano huo, Msigara ameliwataka watendaji wa kata katika halmashauri hiyo kujitambua kuwa wao ndio wakurugenzi katika kata zao, hivyo wanawajibika kwa shughuli zote zinazotokea ndani ya kata.

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ina jumla ya kata 32, vijiji 157 na vitongoji 700 na ina majimbo mawili ya uchaguzi ambayo ni Moshi Vijijini na Vunjo.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo (wa pili kulia), akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga (wa tatu kulia), pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Athumani Masasi, wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa hospitali ya wilaya katika eneo la Mlowa juzi. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Maagizo ya Jafo yaanza kufanyiwa kazi

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

MAAGIZO ya kuanza kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino haraka yaliyotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, zaidi ya wiki moja sasa yameanza kufanyiwa kazi.

Maagizo hayo yalitolewa na waziri huyo baada ya kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa hospitali hiyo inayojengwa katika Kata ya Mlowa, wilayani Chamwino mkoani hapa kusuasua wakati tayari fedha zilishapokelewa zaidi ya miezi mitano iliyopita.

Waziri Jafo amerejea tena katika eneo la ujenzi wa hospitali hiyo na kushuhudia ukiwa unaendelea kwa kasi na majengo zaidi ya matatu yakiwa yameshaanza kupanda na mengine yakiwa yanakamilishwa kwenye hatua ya jamvi.

Mafundi wa kutosha wakiwa wanaendelea na shughuli za ujenzi katika eneo la Mlowa, huku Menejimenti ya Chamwino nayo ikitoa mwongozo wa nini cha kufanya sambamba na Kamati ya Ulinzi na Usalama, ikiwa inahakiki kuwa kila kitu kinaenda kama kilivyopangwa.

Hali hiyo imemfanya Jafo kurejesha imani na halmashauri hiyo kuwa wamejipanga kukamilisha jengo hilo ndani ya muda kama alivyoagiza.

Akizungumza katika ziara hiyo Jafo alisema amefurahi kuona ujenzi wa Hospitali ya Wilaya umefikia katika hatua nzuri na kuwataka watendaji wa Chamwino kuendelea na kasi hiyo ili iweze kumalizika mapema na katika viwango bora.

"Leo naweza kuwapongeza mmefanya kazi kubwa ndani ya wiki moja niliyowapa, sasa nataka ikifika tarehe 12 Mei majengo ya hospitali hii yawe yamefikia hatua siyo chini ya lenta kwa majengo yote saba tayari kwa kuezeka na kuanzia tarehe 25 Mei, majengo yote yawe yamepauliwa," alisisitiza Jafo.

Wakati huo huo, Jafo ameugiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuanza kupanga wilaya hiyo kwa mujibu wa sheria za mipango miji ili uweze kuendana na hadhi ya makao makuu ya nchi.

"Chamwino iko karibu sana na Jiji la Dodoma na jiji hivi sasa wanaenda kwa kasi sana katika upangaji wa maeneo, wanapima viwanja wanauza na wanaongeza mapato yao, lakini sioni jitihada katika wilaya hii na nyie ndiyo sehemu Ikulu imejengwa mnatakiwa mjiongeze muanze kupima maeneo na kuuza ili mwongeze mapato ya halmashauri yenu," alisema Jafo.

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilipata Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya mapema mwezi Oktoba, mwaka jana na hadi sasa unaendelea.

# Wenye ualbino washauriwa kuepuka utegemezi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha watu wenye ualbino (TAS) kimeshauriwa kuibua miradi ili kuondokana na utegemezi unaowafanya kuwa maskini ikiwa ni pamoja na kuungana ili kuunda vikundi vitakavyowawezesha kupata mikopo toka taasisi za kifedha.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Grace Products LTD Dk. Elizabeth Kilili, alipokuwa akizungumza na wanachama wa chama cha walemavu wa ngozi Mkoa wa Dodoma, wakati wa ugawaji wa mafuta na sabuni kwa ajili ya kulainisha na kuondoa madoa kwenye ngozi jijini Dodoma.

Aidha, chama hicho kimetakiwa kufanya kazi kwa bidii na malengo ili waweze kujiinua kiuchumi.

Alisema ili waweze kufikia malengo hayo yote wao wenyewe wanatakiwa kutojikataa kutokana na maumbile kwa kujiona kama hawafai mbele ya watu wengine wasiokuwa na ulemavu huo.

"Ninawaomba mfanyekazi kwa ubunifu na msifanye kwa mazoea, kwa maana mkifanya kazi kama kawaida mtaendelea kuwa maskini na siku zote mtakuwa watu wa kuinyoshea serikali kuwa haiwatendei haki zenu za kimsingi wakati siyo kweli," alisema.

Awali Katibu wa TAS, Hudson Seme, alisema watu wenye ualbino wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikisababisha kuwapo kwa umaskini miongoni mwao.

Alisema hali hiyo imechangia wengi kushindwa kutunza ngozi zao hali inayowafanya kuwa na saratani ya ngozi.

"Moja ya changamoto tunayokabiliana nayo ni hili tatizo la kuwapo kwa umaskini kwenye familia tunazoishi nazo ukizingatia zilizo nyingi zina tatizo la kiuchumi na ndiyo maana tunashambuliwa na magonjwa hayo," alisema.

Katibu huyo pia aliwataka Watanzania kuwajali watu wenye ulemavu kuwasaidia mahitaji muhimu kama vitendea kazi ili waweze kujisimamia wenyewe.

# Serikali kutoa motisha kwa walimu wanaofaulisha

**Na Ibrahim Joseph,** KONDOA

SERIKALI imesema itatoa motisha kwa walimu wa shule zake ambazo wanafunzi watafanya vizuri katika taaluma hususani kwenye ufaulu wa mitihani ya kitaifa.

Kauli hiyo ilitolewa hivi karibuni na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Tixon Nzunda, wakati akifunga mafunzo endelevu kwa maofisa elimu kata wa mikoa ya Dodoma na Singida yaliyofanyika wilayani Kondoa.

Dk. Nzunda alisema serikali itatoa motisha kwa walimu ambao wanafunzi wao watafanya vizuri katika taaluma hasa kwenye ufaulu mzuri kwenye mitihani ya kitaifa.

"Motisha itatolewa kwa walimu ambao wanafunzi wao watafanya vizuri katika taaluma, hususani ufaulu mzuri katika mitihani ya taifa.

Dk. Nzunda aliwataka walimu kote nchini kufanya kazi kwa bidii ili kuwawezesha wanafunzi wanaosoma kwenye shule zao kufaulu kwa kiwango cha juu.

Aliwataka maofisa elimu kata kufanya ufuatiliaji wa karibu na kuhakikisha walimu wakuu wa shule husika wanasimamia taaluma kwa bidii.

Aidha, alisema serikali imekubali kutengeneza mkataba wa utendaji kazi kwa kila mwalimu mbali na mfumo wa Opras.

Alisema kila mwalimu anatakiwa kuwa na maandalizi timilifu muda wote awapo shuleni mfano azimio la kazi , andalio la somo na analofundisha pamoja na mpango kazi wa kuongeza ufaulu kwenye somo analofundisha kwa muhula mzima wa masomo.


Alisema mwalimu atapimwa kutokana na idadi ya vipindi kwa muhula mzima wa masomo hali itakayosaidia kuondoa uzembe kazini.

Alisema kipimo kingine cha mwalimu ni kuongeza ufaulu katika somo analofundisha kupitia majaribio ya kitaifa ya darasa la kwanza na la pili, katika eneo la Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na matokeo ya mitihani ya darasa la nne na saba.

Kwa upande wake, msimamizi mkuu wa mafunzo hayo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Elimu Bagamoyo (ADEM), Lucas Mzelela, alisema mafunzo hayo yanalenga kuboresha kiwango cha elimu nchini.

Mzelela alisema baada ya mafunzo, maofisa elimu kata kwa kushirikiana na wadhibiti ubora elimu, maofisa elimu taaluma wilaya wataenda kuendesha mafunzo hayo kwa walimu wengine katika maeneo yao.

Aidha, alisema chuo hicho kimepewa jukumu la kuendesha mafunzo hayo nchi nzima na serikali kuhakikisha kuwa watoto wote wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika katika kiwango.





# TRA yafafanua fedha za makusanyo ya Zanzibar

**Na Rahma Suleima,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema kwamba fedha za kodi zinazokusanywa Zanzibar kutoka kwa wananchi na wafanyabiashara zinabakia Zanzibar kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Hayo yalisemwa na Ofisa kodi wa mamlaka hiyo, Omar Abdalla Kirobo, alipokutana na masheha pamoja na madiwani kuwaeleza kuhusu umuhimu wa kulipa kodi.

Alisema ipo dhana ya baadhi ya watu wakiwamo wafanyabiashara kwamba fedha za kodi zinazokusanywa Zanzibar jioni hupelakwa Tanzania Bara kwa matumizi ya huko.

"Sio kweli, fedha za kodi zinazokusanywa Zanzibar zinabakia hapa na kutumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwa wananchi wa Unguja na Pemba," alisema Korobo.

Ofisa huyo alieleza kwamba nchi haiwezi kupata maendeleo na kutekeleza miradi ya jamii kama wananchi na wafanyabiashara watashindwa kulipa kodi inayostahiki kwa mujibu wa sheria.

Naye Ofisa wa Elimu ya Kodi na Huduma kutoka mamlaka hiyo, Abdalla Seif, aliwataka viongozi wa shehia wakiwamo masheha na madiwani kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema bado wapo watu wengi wenye sifa wakiwamo wafanyabiashara ambao hawalipi kodi kwa mujibu wa sheria.

"Mamlaka ya mapato nchini bado inawataka wananchi na wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati bila ya kushurutishwa kwa sababu kodi inatumika katika shughuli za maendeleo," alisema.

Baadhi ya madiwani na masheha waliitaka mamlaka kutoa elimu zaidi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ili jamii ifahamu malengo yake.

"Tatizo moja kubwa jamii yetu haifahamu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya taifa, lakini na taasisi za mapato nazo zitoe elimu zaidi," alisema Khatib Chwaya, ambaye ni sheha wa Wete Pemba.



Mafundi wakijenga jengo la maabara ya kisasa ya huduma za afya ya Kanisa Katoliki, Parokia ya Bukima, Musoma Vijijini, mkoani Mara juzi, ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wanawake CCM waaswa viti maalum, kuteuliwa

**Na Rahma Suleima,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Kusini Unguja, wametakiwa kuwaunga mkono wenzao wanaojitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Imeelezwa kuwa kwa kufanya hivyo, hatua ya kufikia uwakilishi wa asilimia 50 kwa 50 itafikiwa, hivyo kuacha kutegemea nafasi za kuteuliwa na za viti maalum.

Wito huo ulitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo Zanzibar, Tunu Juma Kondo, alipokuwa akizungumza na wajumbe hao katika ziara ya kujitambulisha na kuangalia uhai wa chama hicho katika wilaya hiyo.

Alisema wanawake wengi wanajitokeza kugombania nafasi za uongozi, lakini wanashindwa kuchaguliwa kutokana na kutoungwa mkono na wanawake wenzao.

Alieleza kuwa zama za kutawala mfumo dume zimepitwa na wakati, hivyo ni kwa wanawake kuwaunga mkono wanawake wenzao ili kuingia kwa wingi katika vyombo vya kutunga sheria kupiga vita masuala ya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Kusini Unguja, Mwantatu Mbaraka Khamis, aliwataka wanawake hao kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zinazotolewa na serikali ili waweze kujitegemea katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Kwa upande wao, wajumbe wa jumuiya hiyo, waliahidi kuvifanyia kazi vipaumbele vya wanawake vilivyowekwa ikiwamo kuingiza wanachama wapya kutoka makundi mbalimbali kama ya wakulima, wafanyakazi na wajasiriamali kwa lengo la kuendeleza jumuiya hiyo.

# Nyavu zawatia matatani wavuvi

**Na Rahma Suleima,** ZANZIBAR

WAVUVI 20 kutoka Kijiji cha Fukuchani Mkoa wa Kaskazini Unguja, wamekamatwa na maofisa wa Idara ya Uvuvi wakivua samaki kwa kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo zimepigwa marufuku.

Mwanasheria wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Zanzibar Mwinyi Mataka Mwinyi, alisema wavuvi hao wamekiri kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo hazifai kwa matumizi ya uvuvi ambazo hunasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Alisema Sheria ya Uvuvi Na. 10 ya mwaka 2010 imepiga marufuku aina zote za uvuvi zinazotumia nyavu zenye macho madogo ambazo ni hatari kwa mazingira ya bahari na samaki kwa ujumla.

"Uvuvi wa kutumia nyavu zenye macho madogo haukubaliki kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 10 ya mwaka 2010, ambao athari zake kwa uharibifu wa mazingira baharini ni kubwa," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini Unguja, Hassan Ali Kombo, alisema sheria za uvuvi zinakataza kutumia nyavu zenye macho madogo kwa shughuli za uvuvi huo.

Aidha, alisema uvuvi wa kuzamia kwa kutumia bunduki pia umepigwa marufuku kwa mujibu wa sheria za uvuvi kutokana na athari za uharibifu wa matumbawe.

Aliwataka wavuvi kuacha mara moja kujishughulisha na aina hizo za uvuvi kwa sababu adhabu yake ni kubwa ikiwamo kutaifishwa kwa chombo cha uvuvi. "Serikali imepiga marufuku uvuvi wa kutumia nyavu zenye macho madogo ambazo miongoni mwa athari zake ni kunasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula," alisema.

Mvuvi mmoja aliyejitambulisha kwa majina ya Daud Juma Ali alikiri kutumia nyavu ndogo kwa matumizi ya uvuvi na kuomba radhi kwa kosa walilotenda.

"Mheshimiwa, tunaomba radhi kwa kosa la kutumia nyavu zenye macho madogo kwa shughuli za uvuvi," alisema.



**FRESH KID HUKU SHULE, HUKU JUKWAANI**

Soma UK.19

JUMAMOSI APRILI 20, 2019

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# Kumbe Pam D unaheshimu mashabiki!

BASI SAWA



## Belle 9 fyekelea mbali skendo

MSANII Belle 9 amesema amedumu katika muziki kwa miaka 11 sasa bila kukumbwa na skendo yoyote, kwa madai kwamba hazina nafasi kwake.

"Skendo siyo sehemu ya maisha yangu, na haitatokea siku moja nifanye jambo la ovyo ili nipata umaarufu, ninamheshimu Mungu na muziki wangu," amesema Belle 9.

Amesema amechagua kuishi maisha ya aina hiyo, ambayo yamemfanya aendelee kuwa na heshima kubwa mbele ya jamii, hivyo haoni ni kwanini atumie njia mbovu kujiongezea umaarufu.



## Kazana Mwapwani utafanikiwa

MWIMBAJI Mwapwani Yahaya amesema anatamani kupiga vyombo mbalimbali vya muziki ili kujiongezea ujuzi kwenye muziki.

"Kwa sasa ninajifunza kupiga violin nikashafanikiwa nitahamia kwingine ili kutimiza lengo langu la kujua kupiga vyombo mbalimbali vya muziki," amesema Mwapwani.

Msanii huyo aliyeibuliwa na mashindano ya Bongo Star Search (BSS), amesema hatua hiyo inaweza kumsaidia kwa baadaye kuunda kundi dogo lenye wasanii wanaojua kupiga vyombo mbalimbali.



# Kumbe Pam D unaheshimu mashabiki!

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Pam D, ameweka wazi kuwa anapenda kuvaa vikaptula vya kiume kwa vile mashabiki wake wanavutiwa navyo.

Lakini anashangaa kusikia baadhi ya watu wakidai kwamba uvaaji wa vikaptula ameuiga kutoka kwa rapa Chemical.


"Mimi na Chemical ni watu wawili tofauti, mwonekano wangu ni wa kibiashara kwani mashabiki wanataka nivae vikaptula," amesema Pam D.

## INSTA-TWITTER





**Siku** zote kuwa mkweli kwa nafsi yako. Lakini daima uwe wazi kujifunza -**Jennifer Kyaka Odama.**



**Katika** hali ngumu na matatizo ndipo mashujaa huzaliwa. New Manchester itazaliwa baada ya msimu huu - **Nikki wa Pili.**



## Hongera kwa jukumu hili Chuchu

KIMWANA Chuchu Hans ameamua kuibua vipaji vya wasanii wanaochipukia na sasa anamsaidia msanii Renzo kukamilisha wimbo uitwao 'Cheche'.

"Wapo pia wasanii wa filamu, wanaendelea kuandaa tamthilia mbili zenye majina ya 'Nanga' na 'Play Boy', wote hao wako chini ya kampuni zangu za Chuchu Double Touch na Front," amesema Chuchu.

Amesema sasa ameamua kutumia kipaji chake kusaidia wengine na kwamba mwaka 2005 aliwahi kuwa Miss Talent, lakini alikuwa hajatumia vizuri kipaji hicho, hivyo baada ya kumaliza kulea, sasa anaibua vipaji.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

UNASEMAAA...

# Haya Thea wape vidonge vyao

MKONGWE wa filamu Thea amesema, wanaodai Bongo Movies imekufa, watasubiri sana, huku wasanii wakiendelea kufanya vitu vyao kama kawaida.

"Huwa ninashangaa kusikia watu wanachonga eti Bongo Movies imekufa, wasanii wawili au watatu wakishindwa kufanya kazi ya filamu haina maana tasnia nzima imekufa? Wenye mawazo hayo watasubiri sana," amesema Thea.

Thea amesema yeye ni mmoja wa wasanii wa kwanza wa kike nchini kupata umaarufu kupitia filamu na hadi sasa anaendelea 'kudunda' kama kawaida.



BODA 2 BODA

# Bora umejiongeza Mwanambilimbi




MCHARAZA kinanda Deo Mwanambilimbi ameachana na kundi kubwa la wanamuziki na kuunda dogo ili kubabiliana na gharama za maisha.

Amesema bendi ya Kalunde anayoiongoza iliundwa na wanamuziki wengi wakati huo, lakini sasa vyuma vimekaza inabidi kujiongeza, kwa kupunguza idadi yao ili kumudu gharama.

"Wanamuziki tuliopo sasa ni saba, Edson anayepiga besi na kuimba, Yuda Almas anapiga solo na kuimba, Husna Kimti anaimba, Joachim Magazine (drums), mimi napiga kinanda na kuimba," amesema Mwanambilimbi.

## INSTA-TWITTER


Tuffollow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Angusha** chini mambo. Weka chini vitu tuache si tutambe - **Lady Jaydee.**



**Sisi** wanaume ni moja ya viumbe tunaoongoza kwa kusema ukweli. Kwa kuthibitisha hili, hebu tuongee ukweli leo hapa. Una michepuko mingapi? - **Man-fongo.**



**Pale** unapomuona 'ex' wako kachokaa chakaliii, kapoteza nuru, yaani - **Amber Lulu.**

# Kuumbe!



## Ndiyo Shishi, komaa na 'brokeni' yako

**Na Adam Fungamwango**

"NITAZUNGUMZA 'broken English' mpaka kieleweke, aibu ya nini? Mimi Mnyamwezi, nazungumza Kiswahili, Kiingereza ni lugha ya kimataifa ipo siku nitawashangaza wanaonicheka."

Haya ni maneno ya msanii wa filamu, muziki wa kizazi kipya na mjasiriamali Shilole.

Mrembo huyo ameweka wazi kutokana na tabia ya watu kumcheka kuwa hajui Kiingereza na amekuwa akipenda kukiongea mbele za kadamnasi, huku akichemka baadhi ya maneno hata kunyoosha sentesi.

Pamoja na kuchekwa kwenye kadamnasi na kwenye mitandao ya kijamii, msanii huyo ameonekana kuweka pamba masikioni na kuvaa miwani ya mbao, akiweka aibu za kike pembeni na kudai kuwa atakomaa hivyo hivyo na wala haogopi.

Anasema ataendelea kukomaa na Kiingereza chake kibovu mpaka kufikia ndoto ya kuwa miongoni mwa watu wenye uwezo wa kuandika na kuzungumza lugha hiyo kwa ufasaha.

Katika mazungumza na msanii huyo, amesema kwenye safari hiyo, hatojali wanaomcheka, kwani lugha hiyo si ya kwanza kwake.

Aidha, ameongeza kuwa imani aliyonayo ni kwamba ipo siku atakuja kushangaza watu atakapotema ung'eng'e na kuwaacha midomo wazi.

"Huwa sisikii aibu kabisa ninapopewa 'mic' na kuzungumza 'broken English' mbele za watu kwa sababu najua ipo siku kitakuja kunyooka tu," anasema.

Julai mwaka jana, Shilole anayetamba kwa ngoma ya 'Ukin'tekenya', alipata fursa ya kusoma lugha ya Kiingereza kwenye shule moja kwa muda wa miezi mitatu.

Alipata fursa hiyo baada ya video zake fupi alizosikika akikosea kuzungumza lugha akiwa katika harakati za kujitambulisha kwa mashabiki wake na kusambaa katika mitandao ya kijamii hasa Instagram.

Maneno haya ya Shishi ipo siku watu watayakumbuka. Waswahili wanasema siku zote 'wenye moyo wa kupenda kujifunza na kuvumilia, ndiyo wanaofanikiwa.'

Shilole amejipambanua kutokuwa na aibu na hii ni sifa kubwa ya wale wanaotaka kujua lugha za watu.

Kitendo cha kutojali kukosea, atakosea tena na tena na hajali kuchekwa mpaka itafikia wakati atajua kabisa, na wale wanaomcheka watakabaki midomo wazi na kutamani kuwa kama yeye.

Hata Wazungu wanapojifunza Kiswahili huongea kwa kukosea, lakini kwa bahati nzuri wao hawachekwi, ila wanaonekana tu hawajakijua, lakini baadaye wanajua.

Wengi wanaocheka au kumbeza Shilole nao pia hawajui Kiingereza, ila wanaona aibu kuongea mbele za watu kwa sababu watachekwa.

Mtu yoyote mwenye aibu kuongea lugha yoyote kwa sababu ya kuogopa kuchekwa ana dalili zote za kutojua kabisa lugha yoyote ile zaidi ya ile anayoijua tangu utotoni.

Kwa sababu mwenyewe hajali kuchekwa, anachojali ni kujifunza na kuelewa, tena akipenda kuongea mbele za watu ambao wengine wanambeza lakini yeye anasonga mbele, ipo siku atasimama mbele za watu na kuongea Kiingereza ambacho kila mtu hatoamini.

Na hapo kila mmoja ndiyo atarudisha kumbukumbu na kugundua kwa nini hakujali kubezwa na kuchekwa.



## Waigizaji wa 5 wakali enzi za Mwalimu

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni burudani ya aina yake miaka ya '70 hadi 90 nchini Tanzania.

Wakati huo hakukuwa na televisheni Tanzania Bara. Kwa maana hiyo hakukuwa na kitu kinachoitwa Bongo Movie, wala wasanii wa aina hiyo. Wakati huo kulikuwa na sinema tu. Yoyote aliyetaka kutazama ni lazima afunge safari kwenda kwenye majumba maalum ya kuangalia sinema hizo, wenyewe wakiita 'picha.'

Majumba maarufu wakati huo jijini Dar es Salaam, enzi za uongozi wa Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, yalikuwa ni Drive In Cinema, Odeon, Avalon, Empire, Empress, New Chox, Cameo na mengine.

Mastaa wa uigizaji Bongo walikuwa ni wale wanaoigiza michezo inayosikika kwenye redio tu. Na redio yenyewe ilikuwa ni RTD.

Walikuwa wakisikika na kufanya kazi nzuri kwenye michezo ya redio, ilikuwa maarufu sana wakati huo, hasa siku za wikiendi.

Ilikuwa si rahisi kuwajua njiani, labda uonyeshwe na mtu anayewafahamu. Orodha yao ni wengi sana, lakini hapa tunawaweka watano waliokuwa maarufu zaidi na kupendwa na watu wengi.

### 1. IBRAHIM RAHA 'MZEE JONGO'

Ndiye mwigizaji wa michezo ya redio aliyekuwa maarufu zaidi na kujizolea mashabiki wengi wakati wa utawala wa Baba wa Taifa kuliko mwingine yoyote yule.

Lafudhi yake ya Kizaramo, ikichanganyikana na mizaha, mafumbo, vijembe, akionekana pia kutojua vema kutaja majina ya watu na vitu, ilikuwa burudani tosha wa watu waliokuwa wakimsikiliza.

Mzee Jongo alifariki mwanzoni mwa miaka ya 2000, televisheni zikiwa zimeanza kuingia, yeye mwenyewe akiwa ameshaanza kuigiza michezo kwenye runinga. Hata hivyo hakudumu sana kabla umauti haujamkuta.

### 2. BAKARI MBELEMBA 'MZEE JANGALA'

Kwa bahati nzuri huyu anajulikana hata na kizazi cha sasa kwa kuwa anaonekana kwenye vituo mbalimbali vya televisheni. Lakini alianza kusikika wakati huo kwenye michezo ya redio, ikidhaminiwa na kampuni moja ya vinywaji nchini. Akiwa na lafudhi yake ya Kindengeleko, akijipambanua kuwa ni mzee mbishi, asiyesikia la mtu, anayejifanya anajua kila kitu na kusimamia kwenye kile anachokiamini hata kama anapotoka.

Igizo la 'Niachieni Mwenyewe' akiwa na mtoto wake 'Mshamu', liliondokea kupendwa mno na kumfanya kuwa maarufu zaidi na kuwa na jina kubwa ndani ya nchi.

### 3. FUNDI SAID 'MZEE KIPARA', 'PWAGU'

Ni mzee aliyepata bahati ya kuwa maarufu zaidi kwenye televisheni, licha ya kwamba alianza kuigiza tangu enzi za Mwalimu kwenye redio moja ya RTD.

Alifariki mwaka 2010, akiwa msanii maarufu zaidi, kwani uwepo kwenye kundi la sanaa la Kaole lililokuwa likirusha maigizo yake katika kwenye kituo cha ITV, ulimtangaza sana. Kabla ya hapo alikuwa akiigiza kwenye michezo ya redio na michezo mingi na nafasi zake kubwa zilikuwa zile zenye za utemi au ukorofi na alijulikana kwa jina la 'Kipara.'

Pia alikuwa na rafiki yake msanii Ali Keto aliyekuwa akiigiza kama 'Pwaguzi'. Walikuwa na kipindi chao RTD kilichokuwa kikiitwa 'Pwagu na Pwaguzi.'

### 4. ZENA DILIP 'MAUA'

Ni mwigizaji aliyekuwa maarufu wakati ule akiigiza kama mama au msichana mkorofi au mtoto wa mjini, wengi wanawaita masista du.

Ni mwigizaji aliyekuwa na kipaji kikubwa cha kuongea na maneno ya 'shombo'. Uigizaji wake hautofautiani sana na msanii maarufu hivi sasa 'Bi. Hindu.'

Alikuwa akiwekwa sehemu ambazo alitakiwa kuwakomesha mawifi wenye tabia mbaya. Na alizimudu vilivyo, kwani wale mawifi wenye tabia za kuwaachisha wake wa kaka zao, yeye ndiye alikuwa kiboko yao. Lakini pia wanaume wenye tabia ya kuwaacha wake zao waliochuma nao mali na kwenda kuoa wanawake warembo, alikuwa ndiyo mwisho wa matatizo. Alifariki dunia mwishoni mwa mwaka jana.

### 5. HAMISI TAJIRI 'JANJA/MENEJA MIKUPUO'

Ni msanii maarufu aliyekuwa akiigiza kama mtu mwenye kipato kama vile meneja, mkurugenzi au mtu yoyote mwenye wadhifa serikalini.

Aliimudu mno sehemu hiyo kwani sauti yake, pamoja na kwamba alikuwa haonekani, lakini ukiisikia tu, basi moja kwa moja, lazima ije taswira ya mtu wa aina hiyo.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Matokeo ya 'punguzo la bei' ndio hayo sasa - Mama Nah, Manzese DSM.
2. Walisema wahenga, pombe siyo chai. Unaona sasa mlinzi kalala - Mama Nah, Manzese DSM.
3. Hili joto likiendelea navua mpaka ngozi yangu - Beneali Moussa Beneali, Migombeni Zenji.
4. Si utani, babake alipania sana punguzo la bei la Kwa Mkapa - Elisante Mbunda, Manyoni Singida.
5. Daaah! Huyo lazima atakuwa 'afande' wa walinzi halafu kalewa - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
6. Mambo hayo fanya huko huko Dar, Iringa unapotelea kwenye sufuria - Deo Sanga, Makete Njombe.
7. Babu vipi, viatu vimekuchosha nini? - Adinani Mrutu, Kiwalani DSM.
8. Tatizo la kilevi bila kula nyama - Shirima, Morogoro.
9. Ni pozi tu jamani, wala msinijaribu - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
10. Kwa hili joto la mjini, ngoja nijinafasi kwenye kaupepo - Agatha Mbale, Moro Town.
11. Mbwa huko kijijini, mjini wote watu - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
12. Acha kukoroma na ulevi wako wewe, bisi wako anakuja utafukuzwa kazi - Annah Gumbo, DSM.
13. Mmenilisha biskuti mnashangaa nini nikivaa kama nyinyi? - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
14. Ama kweli mbwa wa mjini wanafaidi, wanavaa mpaka milegezo! - Athanas Gumbo, Mbagala DSM.
15. Leo nimetinga suruali, kesho namalizia koti na tai - Flora, Temeke.
16. Unapoingia Sumbawanga usiwe mjuaji saaana, yatakukuta kama huyu jamaa - Mfaume Mbugi, Mshindo Iringa.
17. Ngoja wezi wanione mlevi, halafu watajua kwa nini nilifanywa kuwa mlinzi - Baby Natasha, Magomeni DSM.
18. Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.
19. Hapa sasa kausingizi katakuja, koti lilikuwa na joto balaa! - Simon Mvungi, Sinza DSM.
20. Ushauri wa bure. Siku nyingine usifakamie pombe za bure - Mama D., Michenzani Zenji.
21. Naona kibarua chake kinaota nyasi hivi hivi. Sio kwa kulewa na kulala huko - Mahija Jumbe, Ngamiani Tanga.
22. Sio siri, pombe za leo zilikuwa tamu sana tatizo hazikuwa na asusa. Ona nilivyolewa - Mahija Jumbe, Tanga.
23. Ulinzi umenishinda, niache nilale - 0654 865 436.
24. Kwa hili baridi la Iringa, bora nilale kwa kuvae suruali na viatu - Abousalim, Singida.
25. Ulivamia vitumbua ukidhani nyama eeeh! Ona vilivyokulewesha sasa - Mariam Beneali, Migombani Zenji.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**




# Kikulacho: Mungu akisema 'no' binadamu si dawa

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine mtu anaweza kupata matatizo na asijue kuwa yanatokea wapi.

Lakini kuna msemo wa wahenga usemao kikulacho ki nguoni mwako.

Maana yao ni kwamba mara nyingi tatizo linalompata binadamu kama ni la kutengenezwa, basi atakayefanya mpango huo atakuwa mtu wa karibu.

Wanaamini kuwa mtu wa mbali si rahisi sana kumfanyia ubaya na hata akifanya hivyo atakuwa amepata msaada kutoka kwa mtu wa karibu.

Mtunzi wa filamu ya 'Kikulacho' amejaribu kuangazia madhila yanayowapata watu kwenye jamii ambayo si ya Mwenyezi Mungu, bali ya kutengezwa na watu wa karibu kwa tamaa na sababu zao binafsi.

Imechezwa na Rahim Sinkala, Ester Mwanyonga, Said Mahamood na Hashim Kambi. Ken na mkewe Ester waliishi kwa raha mustarehe kwa muda mrefu.

Hata hivyo, tamaa ya kimwili ikamwingia mke na kuwa na uhusiano na kijana Said. Baada ya kuchonga asali, mama akataka kuchonga mzinga kwa kumfanyia mipango 'kibenteni' chake awe mfanyakazi kwenye nyumba yao. Ikawa hivyo. Akawa dereva wao.

Ken alitokea kumpenda na kumwamini kijana yule kutokana na kuwa ni mchapakazi hodari. Waswahili siku zote wanasisitiza kuwa penzi haligawanyiki.

Mambo yalianza kubadilika ndani ya nyumba, mama akaanza dharau kwa mumewe, kitu ambacho kilianza kumtia wasiwasi Ken. Mtu pekee aliyemweleza tatizo lile na kumwambia achunguze nyendo za shemeji yake ni dereva. Lakini kumbe anayetakiwa kuchunguzwa ndiye mchunguzaji.

Safari moja huanzisha nyingine, baada ya tamaa ya uzinzi kuwaingia, tamaa ya mali ilianza kupiga hodi mioyoni mwao.

Said na Ester walifanya mipango ya kumuua Ken ili wachukue mali zote. Walifanikiwa kutekeleza mpango huo Ken alipoenda shambani.

Dereva alikuwa ameshalipa majambazi pesa ili wamuue bosi wake.

Kilichofuatia Said na Ester ni kuanza kuuza baadhi ya mali za Ken, ikiwamo nyumba zake kadhaa, kumiliki kampuni zake. Hakukuwa na kificho tena, waliishi kama mtu na mkewe.

Isivyokuwa bahati, majambazi wale hawakuikamilisha kazi yao kwa ufasaha. Walidhani wamemuua, kumbe sivyo. Mkulima mmoja alifanikiwa kumchukua na kumpeleka nyumbani kwake, akamtibia kwa dawa za kienyeji hadi alipopona. Baada ya mwezi mmoja alipona kabisa na kuamua kurudi nyumbani.


Hata hivyo, hakuelekea moja kwa moja nyumbani kwake. Alikwenda kwa rafiki yake ambaye alimweleza kila kitu kilichotokea baada ya yeye kuaminika kuwa ameuawa.

Siku chache baadaye Ken anavamia nyumbani kwake na kumkuta dereva wake alikuwa na mkewe. Anachofanya ni kumchapa risasi ya mguu na kumtimua. Anamsamehe mkewe kwa masharti. Baada ya siku kadhaa kila kitu kinarudi kwenye mikono yake, ikiwamo kampuni zake zilizokuwa zimebadilishwa hata majina.

Siku moja Ester anapata taarifa kuwa 'kibenteni' chake kimejinyonga baada ya kuishi maisha ya wasiwasi na ombaomba akiwa mlemavu wa mguu. Naye anaamua kujiua baada ya kugundua pia alikuwa na ujauzito wa dereva.

# FRESH KID

## Huku shule, huku jukwaani



RAPA matata japo mtoto Patrick Ssenyonjo aka Fresh Kid, amepata ufadhili mnono kutoka kwa matajiri wenye asili ya India, Ruparelia Group of Companies, waliowekeza huko Uganda ambao wametangaza kugharamia masomo yake ya shule ya msingi, kwenye moja ya shule kali sana za Kampala.

Rajiv Ruparelia, mtoto wa taikuni au bilionea mwenye kampuni hizo anayetajwa kwa jina la Sudhir Ruparelia, alithibitisha kuwa dogo atamwagiwa fedha ili aendelee na masomo.

"Leo nimekutana na Fresh Kid – rapa matata tena mtoto. Nilivutiwa mno na mafanikio yake, akiwa na umri wa miaka saba anafanya mambo makubwa. Ningependa kumuona akiendelee kusonga mbele akiwa kiongozi na mtia hamasa (inspiration) kwa watoto wengine na vijana wengi zaidi, kwa hiyo Ruparelia Foundation, inampa dogo huyu nafasi ya kugharamiwa elimu yake. Hivyo Ruparelia Foundation, inamlipia masomo yake kwenye shule ya Kampala Parents School."

Hatua hiyo inakuja muda mfupi, baada ya Waziri wa Maendeleo ya Vijana, alipoeleza kuwa mtoto huyo mwenye kipaji cha hali ya juu cha uimbaji apelekwe shule ya bweni. Hata hivyo wazazi, wapenzi na mashabiki zake hawakufurahishwa na pendekezo hilo kwa hofu kuwa kipaji chake kitaathiriwa.

Fresh Kid alitisha kwa kutunga wimbo mkali wa Banteeka akidai wanamuonea wivu kwa sababu ya umri wake mdogo na mwingine unaitwa 'Bambi' akimwomba Waziri wa Maendeleo ya Vijana amruhusu kuimba majukwaani.


Awali Waziri Nakiwala Kiyingi, aliagiza rapa mtoto huyo aache kutumbuiza majukwaani na aendelee na masomo, jambo lililoleta sintofahamu na migongano kwenye mawasiliano ya mitandao ya kijamii. Hata hivyo akaagiza atumbuize nyakati za wikiendi pekee.

Hata hivyo akaanza kupuuza maelekezo ya waziri na kupanda jukwaani nyakati zote bila kujali ni Jumatatu au Jumatano na kumwacha kiongozi huyo kinywa wazi, lakini akibakia kusisitiza kuwa Kid apelekwe shule ya bweni.

Hata hivyo Fresh Kid, amesisitiza kuwa hataki kwenda kwenye shule ya bweni, maamuzi yanayoungwa mkono na wazazi wake wakisema bweni si mahali salama kwa mtoto wao mwenye kipaji kikubwa.

Mtoto Fresh Kid ana bahati ya mtende kwani alipotinga studio kurekodi kibao cha Bambi, alipata ofa za kumsaidia kurekodi video kazi ambayo ni ngumu na si rahisi wengine kuipata.

# Taylor Swift kama Mo Salah



NYOTA wa Liverpool ya Uingereza Mo Salah, ametajwa na kijarida cha TIMES Magazine la Marekani kuwa ni mtu maarufu sana duniani kwa mwaka 2019.

Mo mwenye miaka 26, na ambaye ni raia wa Misri alitajwa na gazeti hilo na kuwekwa juu ya jalada la gazeti hilo kama nyota na mtu maarufu duniani.

Wengine ni mwimbaji Taylor Swift, Sandra Oh, gwiji la miel  ekea duniani 'The Rock' Dwayne Johnson, Spika wa Bunge la Marekani Nancy Pelosi na mtangazaji wa TV nchini Marekani Gayle King.



## Churchill muzee ya pesa nyingi

CHURCHILL aka Mwalimu King'ang'i, mzee wa kupiga shoo kali za kifutuhi, ni moto ana ukwasi –'mafweza' mbaya japo anafanya siri, lakini maonyesho yake ya vichekesho na vunja mbavu yanamletea mamilioni, fedha zinazoingia kupitia matangazo anayoshirikishwa na kampuni mbalimbali na kuuza na tiketi kwa ajili ya onyesho moja.

Comedian huyo anaweza kutajwa kuwa ana hela chafu.

## 'Wakeii' wanaotisha kwa mshiko

MWAKA unaanza vizuri kwa wasanii wa Kenya kuchezea mapesa kama watakavyo. Katika chati za sasa baadhi ya mabilioni hao wanaotisha kimkwanja tunavyojikita ndani ya mwaka 2019 ni; mrembo Akothee ni hatari pesa kama zote.

Hakamatiki. Ni msanii matata na tajiri namba moja ambaye amewekeza kwenye muziki, kampuni za kusafirisha na kuhudumia watalii, makasiri ya kisasa na ardhi akiwa na makasiri ya kisasa yaliyojengwa ng'ambo, mengine yako Mombasa, Nairobi na nyumbani kwao mkoa wa Nyanza.





## We Omondi umelishwa limbwata nini?

MKOMEDIAN mwingine ni Eric Omondi, ananuka utajiri, hivi karibuni alinunua Mercedes Benz mpyaa mbili moja yake na ya mkewe.

Eric, anapata mamilioni kutoka kwenye matangazo kwani anatumika mara kwa mara, kualikwa kuburudisha kwenye hafla kubwa za wazito, kutoa buruduni kwenye mambo ya kitaifa na kimataifa na kwa ujumla ni tajiri anayenufaika kupitia uwezo mkubwa alionao kwenye kutumia tasnia ya habari na mawasiliano.

Kwa ujumla ni miongoni mwa makomediani matajiri kupindukia nchini Kenya.

## Tuzo ya Woods yamwinua Trump

RAIS wa Marekani, Donald Trump, hajaficha siri na kueleza kuwa amefurahishwa na mkongwe wa gofu Tiger Woods, kwa jinsi alivyofanya shoo kali kwenye mashindano ya golfu almaarufu The Masters, lakini pia alivyorejea kwenye gemu baada ya mikasa, kashfa na changamoto nyingi zilizofika kwenye taaluma hiyo.

The Presidential Medal of Freedom, inamaanisha tuzo inayotolewa kwa raia yeyote wa Marekani au wa taifa lolote aliyefanya mambo makubwa, na kufanikisha mchango wa maendeleo ya taifa iwe kwenye usalama wa taifa au dunia, kutetea maslahi ya taifa, kufanikisha masuala ya amani duniani, kuendeleza utamaduni na masuala yote yanayowagusa Wamarekani na dunia pia.





## Mionzi ya Sheria

Na John Juma
0716217615

# Sheria zinavyolinda stahiki mwajiriwa akitimuliwa kazini

KISHERIA zipo sababu mbalimbali, ambazo kwa namna moja au nyingine, zinachangia kubatilishwa mkataba wa ajira baina ya mwajiri na mwajiriwa. Msingi wa mambo hayo, umejengwa katika Sura ya 366 ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya Mwaka 2004.

Mkataba wa ajira, kama ilivyo desturi kwa mikataba mingine kwa mujibu wa sheria, huzaliwa, huishi na kufa; kama ilivyo kwa binadamu na viumbe hai vingine.

Unazaliwa mara baada ya mwajiriwa na mwajiri kutia saini zao. Hapo ndipo wanapouanzisha, utekelezaji wake unapoanza kuchukua hatua na kifo ni pale tu yanapoanza kujitokeza baadhi ya mambo au masuala yanayoainishwa na sheria.

Aidha, zipo taratibu maalum za kumaliza au kuua mkataba wa ajira na hii ni katika mazingira yote, iwe kwa hiari na yale ya kumaliza kwa kulazimika kulingana na sababu mbalimbali.

Kumalizika au kukoma mkataba wa ajira kwa hiari au kufikia ukomo wa kazi kulingana na wepesi wa kutekeleza majukumu ya kazi yenyewe.

Kanuni ya 4 (1)-(7) na ya 5 (1)-(5), zote ni Kanuni za Ajira na Mahusiano Kazini, Kanuni za Utendaji Bora za Mwaka 2007, zinaeleza hakuna shida kama ilivyo kumaliza, kukoma mkataba wa ajira kwa kulazimika kutokana na sababu mbalimbali za kinidhamu.

Katika uhusiano kazini, jambo mojawapo linalomfukuza mtu kazi au kusababisha kukoma mkataba wa ajira, ni utovu wa nidhamu. Hiyo ni mojawapo, kati ya sababu za msingi zinazoweza kumfanya mwajiriwa au mfanyakazi kupoteza ajira yake.

Kimsingi, kanuni hizo zinaelekeza kuwa ni sahihi kumfukuza mfanyakazi kwa sababu za kinidhamu, lakini haimaanishi kuwa mwajiri amtafutie mwajiriwa kisa cha kuzusha au kupika, ili kumwondoa kazini.

Kinachosisitizwa hapa, ni lazima sababu hizo ziwe zimejitokeza na kuthibitika kweli na ziweze kuthibitishwa pale itakapotakiwa kufanyika hivyo. Ujenzi wa hoja kwa kushikilia mkazo kuwa nilisikia au nahisi, zitasababisha tuhuma hizo kukosa mashiko mbele ya msuluhishi, hakimu au jaji kutegemeana na shauri lilikofika.

Kanuni ya 8 (1)(d) na 12 (1)-(5), zote za Ajira na Uhusiano Kazini na Kanuni za Utendaji Bora za mwaka 2007, sanjari na Kifungu cha 37 (2), Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, 2004 Sura ya 366, zote zinasisitiza ukweli na uthibitisho wa madai yanayotolewa. Angalizo ni kwamba, sheria inaelekeza kuwa mwajiriwa au mfanyakazi, atafukuzwa kazi mara moja, bila ya hata kupatiwa barua ya onyo kwa kosa la mara ya kwanza au "summary dismissal".

Kwa utaratibu huo, imafanya mwajiriwa, au mfanyakazi kupoteza haki zake zote za msingi kama kiinua mgongo. Kifungu cha 42 (1)-(4) cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004 Sura ya 366 inalifafanua hilo.

Hivyo basi, ni kosa kwa mwajiri kumfukuza mfanyakazi kwa utaratibu wa mara moja, yaani 'summary dismissal, isipokuwa kama hilo litafanyika katika mazingira ambayo sheria inaruhusu wazi kufanya hivyo na siyo kinyume chake.

Kifungu cha 41 (1)-(7) cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya 2004 sura ya 366 ina ufafanuzi.

**HAKI YA KUSIKILIZWA**

Kila mtu ana haki ya kusikilizwa, kabla hatua ya kisheria kuchukuliwa. Ni haki ya asili, ambayo haiwezi kuondolewa na mtu au mamlaka yoyote ile. Kwa maana hiyo, pasipo kujali ukubwa wa kosa, hata kama kosa la mwajiriwa, mhusika anapaswa kupewa nafasi ya kutoa utetezi wake. Atajitetea na kutakiwa kuwasilisha utetezi wake, dhidi ya: "Kwanini asichukuliwe hatua za kinidhamu?" Kanuni ya 13 (1)-(13) Kanuni za Ajira na Uhusiano Kazini, 2007 inaeleza.

Ni kosa kwa mwajiri au mkuu wa kazi kumfukuza mfanyakazi, bila ya kumpatia nafasi ya kumsikiliza au kujitetea. Hii siyo hiari ya mwajiri kuamua kumpatia mwajiriwa haki husika, bali ni haki ya msingi. Hiyo ni kwa sababu, haki yenyewe ipo kwa mujibu wa sheria, hivyo utekelezaji wake ni lazima.

**HAKI YA MALIPO STAHIKI**

Kifungu cha 44 (1)(a) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, Sura ya 366, kinaelekeza haki za msingi alizo nazo mwajiriwa atakayefukuzwa kazi, kutokana na sababu za kinidhamu. Hiyo ni pamoja na kulipwa mshahara au ujira wake.

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia tarehe ya mshahara wa mwisho mpaka siku ambayo mwajiriwa amefukuzwa, mathalan kama tarehe ya mwisho ya kupokea mshahara itakuwa Juni 30, 2019, kisha mhusika atafukuzwa Julai 17, 2019; pesa itakayotolewa ni kwa kuzingatia siku ambazo mhusika amefanyakazi. Yaani jumla ya siku 17 kuanzia tarehe 1 hadi 17 Julai. Inatajwa kuwa haki ya msingi, wala isipuuzwe kulinda maslahi ya pande zote mbili.



## Kalamu ya Mwalimu

Reubeni Lumbagala

# Ndugai anapodhihirisha umuhimu wa vitabu na matumizi yake

NUKUU zinazowahamasisha watu kukimbilia kusaka maarifa kwenye vitabu, ni pamoja na hizi: "A book is a gift, you can open again and again," ikimanisha kitabu ni zawadi unayoweza kuifungua kila wakati." Huyo ni mwanazuoni - Garrison Keillor.

Msomi mwingine, Harry S. Truman, anatamka kwa kiingereza tena: "Not all readers are leaders, but all leaders are readers." Tafsiri yake ni kwamba: "Si wasomaji wote ni viongozi, lakini viongozi wote ni wasomaji."

Ili mtu awe wa kipekee katika sura ya kuanzia kiongozi, mbobezi na mtu maarufu, ni lazima kusoma vitabu. Ndiyo maana, Spika wa Bunge , Job Ndugai, ambaye ni Mbunge wa Kongwa, ameamua kusaka vitabu kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wa shule za wilayani Kongwa, kuwaongeza maarifa kikamilifu.

Kwa ujumla, vitabu ni nyenzo muhimu inayofanikisha kujifunza na ufundishaji wa wanafunzi na wengine popote. Kupitia vitabu viliyoandaliwa na wataalamu, wasomaji hupata maarifa mbalimbali yanayoibua uelewa, ujuzi na kubadilisha maisha, yawe katika hali bora zaidi.

Hivyo basi, kila anayetaka kujifunza masuala mbalimbali, hana budi kusoma vitabu vingi, ajiongeze ujuzi na kupata utajiri wa maarifa.

Wasomi na waandishi wa vitabu, wanaamini kuwa ubongo wa mwanadamu unahitaji kulishwa chakula, ili uweze kufikiri vyema na njia pekee ya kuulisha ubongo ni kusoma vitabu mbalimbali. Ndiyo maana vitabu vinaitwa 'chakula cha ubongo.'

Kwa kutambua umuhimu wa vitabu katika kujifunza na ufundishaji wenye tija shuleni, Spika Ndugai, hivi yuko katika jitihada za kuzitafutia shule za sekondari wilayani Kongwa, vitabu vya kiada na ziada, kwa wanafunzi na walimu, wapate maarifa ya kutosha.

Mbunge huyo ameshatembelea shule za sekondari wilayani Kongwa kuvifikisha vitabu hivyo, akiongozana na viongozi wa wilaya hiyo ambao ni; Kaimu Ofisa Elimu wa Wilaya, Emmanuel Factory, Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wa Wilaya Kongwa, Andrea Nyemba na katibu wake, Ramadhani Tessua.

Mmano tarehe 18, zilizopita, alizuru katika sekondari za Chiwe, Mlali, Ndurugumi na Kibaigwa, alikopata wasaa wa kuongea na wanafunzi na walimu, akiwahimiza wanafunzi kusoma kwa bidii, ili kufanikiwa maishani. Baada ya kuongea na jumuiya za shule hizo, kazi ya ugawaji vitabu vya kiada na ziada ilifanyika kwa masomo mengi ambayo ni: Fizikia, Kiswahili, Historia, Kemia, Uraia, Baiolojia, Jiografia, Hisabati na Kiingereza.

Mwenyekiti wa CWT, Andrea Nyemba, aliopokuwa Mlali, alisema: "Maarifa hupatikana kwenye vitabu, hivyo wanafunzi wekeni juhudi kubwa, kuyatafuta maarifa kwenye vitabu mlivyopewa na mheshimiwa mbunge".

Spika Ndugai na timu yake walipofikia katika Shule ya Msingi Visumi, alikabidhi fedha taslimu shilingi miolini 2.2, ambayo ni mchango wa CWT makao makuu na shilingi 200,000 kutoka CWT wilayani Kongwa. Zote ni kwa ajili ya kusaidia kupaua darasa.

Machi 23, walikuwa katika Shule ya Sekondari za Banyibanyi, Songambele Kilimani, Hogoro, Ndalibo, Laikala na Ibwaga, sanjari na ugawaji vitabu, suala la michezo alilipa kipaumbele kwa kuzigawia jozi za sare na mpira. Hiyo iliendana na wanafunzi kuhimizwa kucheza, kwa tafsiri michezo ni afya na ajira. Katika Sekondari ya Ibwaga, yenye wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita, Spika Ndugai alichangia kompyuta, 'printa' na mashine ya kudurufu (fotokopi).

Ni misaada inayotolewa katika maana ya kukuza taaluma, shule sasa kunufaika na kudurufu mitihani na majaribio mbalimbali, kwa ajili ya kuwanoa wanafunzi kujisomea mitihani ya taifa ya miaka iliyopita na mahitaji mengine.

Ziara ya kugawa chakula cha ubongo katika shule nyingine zilikuwa: Ngomai, Makawa, Zoissa na Mangh'aila. Huko walikuwa viongozi kadhaa; Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya, Nelson Milanzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kongwa, White Zuberi.

Iwapo wanafunzi watatumia kikamilifu vitabu walivyopewa kwa kuvisoma na kuvielewa, upo uwezekano wa sekondari za Kongwa kufanya vizuri katika mitihani yao ya taifa ya mwaka huu wa 2019.

Ikumbukwe kuwa, mwaka 2017 Wilaya ya Kongwa katika matokeo ya kidato cha nne, ilishika nafasi ya kwanza kwa Mkoa wa Dodoma na mwaka jana nafasi ya pili.

Pia, upatikanaji wa mitihani ya taifa ya miaka ya nyuma, imekuwa changamoto inayowakabili wanafunzi wa shule nyingi za msingi na sekondari mkoani Dodoma.

Vitabu vilivyotolewa na mbunge, ni sehemu ya utatuzi wa changamoto za zinazowakabili wanafunzi wa sekondari za Kongwa, kwani miongoni mwa vitabu vya ziada zilivyotolewa, vimo vyenye maswali ya mitihani ya taifa ya miaka ya nyuma na majibu yake, kwa masomo yote.

Vitabu hivyo ni muhimu kwa wanafunzi katika kuwapatia dira ya namna mitihani ya taifa inavyoandaliwa na inawasaidia kufanya mazoezi ya kutosha, kwa kujipima na kujisahihisha kupitia majibu yaliyomo vitabuni. Ziara ya Ndugai bado inaendelea, ikilenga kukuza taaluma.

●**Mwandishi ni mwalimu katika Shule ya Sekondari Mlali, wilayani Kongwa, Dodoma. Kwa maoni mpigie simu: (+255) 0764 666349.**

# Miaka 10 mjane alea watoto 5 walemavu wasiojiweza kila hali

## ■Wenzake waguswa, wampunguzia mzigo

**Na James Lanka, aliyekuwa Same**



Nighenjijwe Amini Mnjokava (kulia), anayewalea watoto wake watano wenye ulemavu, katika picha ya pamoja na watoto wake, alipotembelewa na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule (wa pili kulia waliokaa) na Mkurugenzi wa Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya Upendo Friends ya jijini Arusha, Isabella Mwampamba (watatu kulia waliokaa). **PICHA ZOTE: JAMES LANKA**

KUNA usemi wa Kiswahili: "Uchungu wa mwana aujuaye mzazi." Hilo liko katika uthibitisho wa matendo kwa mwanamama mjane, Nighenjijwe Mnjokava, mkazi wa Kata ya Chome wilayani Same, Mkoa wa Kilimanjaro.

Ni mama anayewalea watoto watano, wote wenye ulemavu. Hivi sasa ni wastani wa miaka 10 imepita, mwanamama huyo anafafanua kuwa, amekuwa akiwalea watoto wake ambao hawakuwa hata na uwezo walau kwenda kujisaidia, kutokana na hali ya akili na viungo vyao.

"Navishukuru sana vyombo vya habari kwa kuwa baada ya kutoa habari zangu, alijitokeza mwanamama mwenzangu aitwaye, Isabella Mwampamba, akiwa na marafiki zake kutoka Arusha na kuanza kunisaidia katika mahitaji mbalimbali, ikiwamo kuboresha nyumba yangu niliyoachiwa na marehemu mume wangu, ambayo tayari ilikuwa katika hali mbaya sana ya uchakavu," anaeleza.

Mama huyo, anasema kwa kutambua uzito wa kuwalea watoto watano walemavu, Isabella alijitolea kumlipa msaidizi wa kulea watoto hao na kwa sasa ameongeza msaidizi mwingine, hali inayompa ahueni kupata muda wa kujishughulisha na kutafuta riziki.

"Kipekee namshukuru Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ambaye ameungana na juhudi anazofanya mama Isabella kwa kunitembelea Siku ya Wanawake Duniani na kunitia moyo pamoja na kuniletea mahitaji mbalimbali, ikiwamo kunijengea jiko la kisasa na ukuta wa kingo kwa nyumba yangu," anasema.

**MAMA MWAMPAMBA**

Isabella, ambaye ni Mkurugenzi wa Shule ya Upendo Friends iliyopo jijini Arusha, anasema aliguswa kufanya hivyo, baada ya kuona katika vyombo vya habari, mateso hayo ya mwanamama mwenzake.

"Kwanza nilimshirikisha Mungu anipe uwezo na ujasiri wa kumsaidia mwanamama huyo. Nilifunga safari kutoka Arusha hadi eneo la Chome wilayani Same nikiwa na baadhi ya marafiki zangu na kuanza kumpatia kwanza mahitaji ya kibinadamu," anasimulia Isabella.

Anasema, hata aliporudi nyumbani kwake jijini Arusha, alimsimulia mumewe hali duni na mateso aliyomkuta nayo mwanamama huyo safarini Same na walishauriana kwenda kuboresha makazi yake, sanjari na kumjengea jiko la kisasa na wakalitekeleza.

"Pia tulimwongezea msaidizi wa kumsaidia kuwalea watoto wake hao kwa kuwapikia, kuwafulia na kuwaogesha. Hivi majuzi, tumemwongezea msaidizi mwingine.

"Kipekee namshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ambaye pia ni mwanamama mwenzetu kwa kutuunga mkono mimi na marafiki zangu," anasimulia.

"Nakumbuka tulipomtembelea Siku ya Wanawake Duniani, tukiwa tumeambana na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, kumpongeza kwa ujasiri wake aliuonyesha kama mwanamke," anafafanua Isabella na kuongeza:.

"Alifurahi sana na kila mmoja wetu aliahidi kumsaidia kadri ya uwezo wake. Ninamshukuru Mungu, kwani kwa sasa angalau anaishi vizuri.

Anafafanua zaidi kuwa, aliamua kufanya safari ya kupanda mlima Kilimanjaro hadi kileleni, ili kuenzi changamoto anazopitia mwanamama mwenzake kulea watoto wake watano wenye ulemavu, wakichangisha pesa walizomwahidi.

"Kipekee namshukuru sana mwanamama mwenzangu, Zainab Ansell, Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Zara Tours, ambaye alinifadhili safari ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa siku sita," anafafanua Isabella.




Isabella Mwampamba, akiwa juu ya barafu katika kilele cha Kibo Volcanic, katika safari yake ya kupanda Mlima Kilimanjaro, kusaidia watoto watano wa familia moja. Alifanikiwa kukusanya Sh. milioni 7.5

> **"Kipekee namshukuru sana mwanamama mwenzangu, Zainab Ansell, Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Zara Tours, ambaye alinifadhili safari ya kupanda Mlima Kilimanjaro kwa siku sita," anafafanua Isabella.**

Anasimulia kuwa, ilikuwa safari ngumu na yenye changamoto nyingi, lakini aliweza kufika eneo la Kibo na hakufanikiwa kufika kilele Uhuru Peak, umbali wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari kama alivyokusudia.

"Safari yangu ya siku sita kupanda mlima Kilimanjaro ilikuwa ngumu na yenye changamoto nyingi sana, kama baridi na upepo mkali sana, unaoamabatana na theluji. Ila ninamshukuru Mungu kufanikiwa kukusanya kiasi cha milioni nane nilizomwahidi mwanamama mwenzangu," anasimulia mama huyo.

Hiyo inadhihirishwa na umuhimu wao mkubwa walio nao kinamama katika jamii, hasa katika suala la malezi kwa watoto kuanzia wanapozaliwa hadi umri wa kujitegemea. Kwa maneno mengine "Mama ni 'mwalimu wa kwanza' wa binadamu yeyote na katika taifa lolote/"

**●Mwandishi wa Makala haya anapatikana kwa anwani yabarua pepe: jlanka6@gmail.com Simu:+(255) 0752 691 129**



Moja ya ajali mbaya zinazolalamikiwa kila siku, kusababisha vifo, majeruhi na hasara za mali nchini. **PICHA: MTANDAO**

# Wazazi Pasaka isiwe sherehe ya misiba

**Na Mwandishi Wetu**

KESHO ni maadhimisho ya Pasaka. Tunawatakia wasomaji wetu sikukuu njema na ya heri. Lakini, wazazi na walezi wasisahau kuwalinda watoto wao, ili kuwaepusha na ajali zinazotokea kwa kutumia usafiri usio stahiki.

Vifo vinavyoweza kutokea kutokana na ajali za kutumia usafiri wenye mashaka ni pamoja na bodaboda , bajaji, magari madogo na makubwa, ambazo takwimu zake japo hazijatajwa, lakini zinaangamiza maisha ya watoto hasa wakati wa sikukuu kama Noeli, Mwaka Mpya na hiyo ya kesho ya Pasaka.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inayotolewa kwenye hotuba ya bajeti ya mwaka 2018/2019, inasema mwaka 2017ajali 1,584 za bodaboda zilitokea nchini na watu waliouawa ni 763.

Aidha, mbali na kuua majeruhi walikuwa 1,224. Idadi hiyo ya vifo ni kubwa na kwamba maisha yaliyopotea 763 ni ya watu ambao taarifa zao zilifikishwa kwenye vyombo vya usalama.

Bodaboda sasa zimesambaa nchini na zinaongoza kwa idadi ya vifo, mbali na ulemavu wa kudumu, majeraha mbalimbali na uharibifu wa mali.

Takwimu hizo ni kwa ajali zilizoripotiwa polisi tu, bado zile zisababishwa na madereva wa uchochoroni ambao hakuna anayefahamu habari zao.

Sababu za kuwapo ajali hizo ni nyingi wengi wanaoendesha bodaboda hawajafunzwa mafunzo ya udereva. Huenda wengi wao ambao hawana leseni au bima kwa vyombo hivyo tena wakiwa na mihemko ya ujana, wanapenda muziki mkubwa, vilevi na kuna wanaotumia mihadarati.

Wakati wa sikukuu madereva wengi wanajiachia kwa vile pengine kwa kuamini kuwa hakuna askari wa kuwahoji na kuwafuatilia kama inavyokuwa siku nyingine.

Hili si suala la kuwatishia wazazi, walezi au waendesha bodaboda lakini ni muhimu kufuatilia ili kujua kusimama kwenye tahadhari badala ya kufanya mambo kwa mazoea.

Ni vizuri pia kufuatilia taarifa za ajali zinazopatikana katika Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), kwani kuna watu wengi wameumizwa na pikipiki na bajaji na watoto pia ni sehemu ya majeruhi hao.

Mwaka jana MOI, ilieleza kupokea majeruhi wa ajali za bodaboda takribani 20 kila siku, na kuufanya uwezekano wa watu 600 kujeruhiwa kila siku na pikipiki.

Ukweli ni kwamba kuruhusu pikipiki na bodaboda kuwasafirisha watoto wakati kama huo wa sikukuu unaweza kufananishwa na kuwatumbukiza kwenye midomo ya mamba.

Pamoja na kwamba sikukuu ni muda wa kupata fursa za kuhudumia wateja wengi, lakini ni vyema kuwalinda watoto, ili fursa hiyo isiwe na athari kwao.

Inawezekana bajaji, pikipiki ambazo ni kama teksi, huku zama zilizopo kuna magari mbadala wa mabasi yakiwamo ya safari ndefu. Si jambo baya.

Lakini, matumizi mabaya ya vyombo hivyo wakati wa sikukuu, ni tatizo. Kwa mfano, madereva wengi wanakunywa pombe nyingi wakati wa sikukuu na kuendesha kwa vurumai.

Masuala kama kubeba abiria zaidi ya mmoja "mshikaki" ni utaratibu unaotumika wakati wa sikukuu nao unaongeza hatari zaidi. Pia, kuna kuwabeba watoto wote au familia nzima kwenye bajaji ni hatari.

Watu wanawapakiza watoto wao zaidi ya wawili kwenye bodaboda na wengine wanashindiliwa ndani ya bajaji. Wazazi na walezi wakumbuke kuwa hata hao madereva wa vyombo hivyo hawako makini.

Hiyo ni kwa sababu wapo 'wanaojilipua' kwa kunywa pombe. Baadhi wanachanganya vileo vya aina mbalimbali. Wapo wanaovuta bangi na mihadarati mingine, baadhi wanatamba 'wamejilipua.' Kwa hiyo, wazazi, walezi na wanafamilia, chungeni watoto wenu.

Inashangaza wakati mwingine, wazazi wanawapakiza watoto pamoja na wa majirani ndani ya bajaji, tena wakiambiwa wabebane na kukaliana.

Hapo kuna uwezekano wa kuwaumiza watoto, hasa pale bajaji zinapoyumba, pia kama dereva amelewa na amefungulia muziki mzito wenye sauti kali.

Kama ningeombwa ushauri, ningehoji hivi ni lazima watoto hawa wabebwe kwenye bajaji na bodaboda, wakati wa sikukuu au muda mwingine wowote?

Pamoja na kwamba, kuna imani na jeuri kuwa hakuna shida kwa sababu serikali imeridhia bodaboda zitumiwe kama vyombo vya kusafirisha abiria kibiashara, hiyo haina maana kuwa watu wasijali maisha yao.

Hata kama ni sheria na kuna ridhaa ya serikali, lakini si suala la kuchezea maisha ya watoto ambao wakiwa kwenye bodaboda hawana kofia za 'helimeti' za kufunika vichwa vyao linawaweka kwenye hatari zaidi.

Sheria isichukuliwe kimasihara, kiasi cha kuhatarisha maisha ya watoto, ambao hawawezi kujitetea ajali zinapotokea.

Waathiriki wa usafiri wa bodaboda, bajaj na magari yenye madereva 'wanaojilipua' na kukimbiza kwa mwendokasi mkubwa wakati huo wa sikukuu, ni watoto na vijana ambao bila ya kujitambua, wanajikuta wakifurahia sikukuu kwa utaratibu unahatarisha maisha.

Wazazi na vijana wanaoaswa kuyafahamu haya na ndiyo madhara ya kufanya mambo, bila ya kutafakari. Wanakurupuka wakiamini, kwamba kwa vile ni sikukuu wanaweza 'ku -enjoy' kwa kutumia usafiri mwepesi na rahisi kama huo.

**NINI KIFANYIKE?**

Wadau mbalimbali wakiwamo asasi za kiraia kama Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), wanashauri serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973.

Sheria hiyo inatajwa kuwa na upungufu kama kukosekana vipengele muhimu vya kulazimisha uvaaji ngumu kwa abiria wa pikipiki na bajaji.

Pa, haitaji haitaji umuhimu wa kuvaa mikanda ya usalama kwa abiria wa mabasi ya mijini.

Hivyo magari kama Noah yanapobeba abiria hawalazimiki kuvaa mikanda hali inayowaweka hatarini zaidi iwapo ajali itatokea.

Aidha, haizungumzii suala la kuendesha wakati dereva anaongea na simu, hali kadhalika haijawabana madereva walevi vilivyo, kwa kuwa dereva anaruhusiwa kutumia kilevi kwa kiwango fulani.

Sheria hiyo ina kila hali ya kuhitaji kubadilishwa kuwalazimisha abiria wote kuvaa mikanda, siyo dereva pekee kama ilivyo kwenye daladala. Idhibiti idadi ya abiria ndani ya daladala na kuweka utaratibu unaolinda wateja na vyombo vya moto.

Hata hivyo ni habari njema, muswada wa sheria uko jikoni kufikishwa bungeni kujadaliwa, kama ilivyosikika katika kikao cha wadau wa usalama barabarani wiki hii.

MAKALA

# UNAFAHAMU MTOTO WA JICHO?

## ▪Pombe, kuvuta sigara, dawa
## ▪Imani ya 'kumcheka mkwe'

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAMU wa afya wanawashauri watu kuepuka matumizi ya tumbaku au sigara, wakihusisha na matatizo mengi ya kiafya kama saratani, kuvimba moyo na magonjwa ya mfumo wa hewa.

Tumbaku inatajwa kuwa kisababishi cha tatizo maradhi ya mtoto wa jicho. Kwa baadhi ya jamii nchini, tatizo hilo huhusishwa na imani kuwa mgonjwa 'umemcheka mkwewe.'

Wanamini kumcheka baba au mama mkwe, kunaleta tatizo hilo, bila ya kujua chanzo ni pamoja na ulevi na uvutaji sigara.

Aidha, watu wanapoonekana wana matatizo hayo, wanahusishwa na madai ya kuwabeza watu au kukonyeza wakubwa zao. Ni maelezo yanayotolewa kwa kila mwenye tatizo hilo, awe mwanamke au mwanaume, pia hata kwa watoto wadogo.

Madai ya kucheka wakwe ni fikra zisizokuwa za kitafiti, lakini zimeendelea kudumu na zimezoeleka katika sehemu nyingi.

**INAANZIA WAPI?**

Nchini Tanzania, mtoto wa jicho si jambo geni na wakati mwingine hupuuzwa, ikihatarisha kusababisha upofu.

Mtoto wa jicho au 'cataracts' inatokea na kukua taratibu kwa miaka mingi. Dalili kubwa ni jicho kuona kwa tabu, na wakati mwingine mtu anauhisi anaona ukungu.

Mara nyingi mtu akiwa na tatizo hilo, unapoangalia huwa anaona kama anachungulia kwenye kioo chenye mvuke au ukungu.

Taarifa za taaluma ya afya, ni kwamba mtoto wa jicho unatokana na kuongezeka protini ndani ya ngozi nyepesi ambayo katika sehemu inayopitisha mwanga jichoni.

Jicho la binadamu, linafanya kazi mithili ya kamera. Kitu muhimu ni mwanga unaingia, baada ya kupenya kwenye kiwambo ama ngozi laini iitwayo 'cornea' ambayo ni ute mwepesi unaofanishwa na majimaji ndani ya yai.

Kwa upande mwingine, kimiminika hicho ni angavu kinaonyesha (transparent) ili kuruhusu mwanga kupenya kwa kasi na mwanga huo unakwenda na kuingia ndani ya lenzi au mboni ya jicho. inayopindisha mionzi ya mwanga ili itue kwenye kitu jicho linachokitizama.

Kazi ya kuona na kukitambua mtu anachotazama, hukamilika baada ya picha yake kufikishwa ubongoni na mishipa ya neva ya kuona ziitwazo 'optic nerves.'

Hizo zinazopeleka taarifa na kutafsiriwa ubongoni na kutoa ujumbe wa kile mtu alichoona, mathalani, mbwa, mmea au bodaboda.

Kitaalamu tatizo hilo linaitwa 'cataract' na inatokea wakati kuna mkusanyiko wa protini kwenye lenzi au mboni ya jicho na kusababisha ukungu au giza linalozuia mwanga kupenya kwenye 'retina' hivyo na kuwa chanzo cha jicho kukwama kupindisha mionzi kutazama kilicho mbele yake.

Protini hiyo ni chembehai zinazojikusanya nje ya lenzi na kusababisha uvimbe ambao pia huathiri seli nyingine zilizo jirani na mboni ambazo hukusanyika na kutengeneza mtoto wa jicho na kulizuia kuona.

Uvimbe huo humkwamisha mgonjwa kuona na kuwa na mwonekana mbaya machoni wakati mwingine macho hufanana na ya mnyama hasa kondoo.

Kwa mujibu wa taarifa za mitandao wa 'MMed' na 'Mayo Clinic' mionzi ya jua iitwayo 'ultraviolet au infra red' inatajwa kuwa inachangia kuharibu mboni ya jicho. Ndiyo maana wengi wanalazimika kukunja uso na kuzuia mwanga usiingie machoni.

**SIGARA**

Pia, uvutaji sigara unatajwa kuumiza mboni ya jicho inayopata misukosuko, kwani wakati mtu anapovuta sigara, moshi unaingia machoni na kusababisha kukunja misuli ya uso, pia jicho lake.

Unywaji pombe nao ni tatizo linalopofusha, kwa kupitia athari kwa mtoto wa jicho, kwa vile inaathiri mifumo ya fahamu inayohusiana na kuona.

Kadhalika uchafuzi wa hali ya hewa, vumbi angani na kwenye maeneo ya makazi yote husababisha jicho kuwa na uvimbe huo.

**UMRI & MARADHI**

Umri nao unatajwa chanzo. Kiasi mtu anavyozeeka, pia kunakuwapo na uwezekano wa protini hizo kujikusanya na kuvimba katika mboni.

Sababu nyingine inatajwa kuwa magonjwa kama kisukari, ambacho huharibu mishipa ya fahamu, ikiwamo ya macho na hata wakati mwingine, kusababisha presha ya macho au 'glaucoma'. Pia, kuna shinikizo la juu la damu.

Kitambi cha mwili ni kisibabishi, vivyo hivyo matumizi ya dawa muda mrefu, kwa mfano vidonge vya kupungunza lehemu mwilini.

**VYANZO VYA KUZALIWA**

Kuna aina za uvimbe unaosababishwa na maambukizi wakati wa ujauzito. Kadhalika, kunatajwa suala la kuumia au afya duni ya mama katika kipindi cha ujauzito, inamwachia mtoto tatizo.

Pia, katika hatua hizo kuna suala la kuathiriwa na kemikali zinazopatikana ndani ya dawa zenye viambato vya 'corticosteroids au diuretics.'

**TIBA IKOJE?**

Mara nyingi watu wakigundua wana mtoto wa jicho, hukimbilia kuvaa miwani yenye mwanga mkali na wapo wanaoamua kutumia miwani yenye lenzi zinazokuza na kuongeza ukubwa wa vitu.

Hiyo inasaidia kufanya vitu viwe na ukubwa zaidi na kupunguza maumivu ya misuli na mishipa ya jicho lenye mtoto, au tabu zinazojitokeza wakati wa kutazama.

Kwa ujumla tiba maalumu na muhimu kwa tatizo hilo kitaalamu inatajwa kuwa ni upasuaji, kwa kuwa inaondoa lenzi isiyopitisha mwanga na kuweka nyingine ya kuchongwa (bandia) na inayomsaidia mtu kuona, kama ilivyokuwa mwanzo.

Nchini Tanzania kuna kliniki nyingi za macho na kuna taasisi za afya zinazowatembelea wananchi mijini na vijijini kuwafikishia huduma ya macho.

Hivyo ni muhimu watu wajitokeze kupima macho, kupewa miwani na kufanyiwa upasuaji wa jicho bure au kwa gharama nafuu.

**●Makala hii inatokana na mtandao wa MMed na Mayo Clinic.**



Mgonjwa wa mtoto wa jicho. Picha nyingine, matibabu ya ugonjwa huo. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**





HABARI KIMATAIFA

## Ufaransa yakanusha tuhuma za kuusapoti upinzani Libya

**TRIPOL,** Libya

UFARANSA imekanusha vikali madai ya Libya kuwa inamuunga mkono Kamanda wa kijeshi Khalifa Haftar, anayeongoza vikosi vyake kujaribu kuliteka Jiji la Tripoli.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Libya, Fathi Bach Agha, ametangaza kusitishwa kwa uhusiano kati ya serikali yake na ile ya Ufaransa kwa madai ya kuwaunga mkono maadui wake.

Wakari huo huo, wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wameanza majadiliano kuhusu namna ya kuwezesha pande zote mbili kusitisha mapigano.

Wiki iliyopita, Kanali Mohamad Gnounou, msemaji wa vikosi vya serikali ya umoja wa kitaifa inayotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa (GNA) alishutumu vikosi vya Jenerali Khalifa, kuweza kuingia sehemu ya mji.

Hata hivyo, mapigano bado yanaendelea pembezoni mwa Mji wa Tripoli ambapo baadhi ya raia wa maeneo hayo wameyakimbia makazi yao. **RFI**

## Serikali ya Mali yajiuzulu

**BAMAKO,** Mali

RAIS wa Mali, Ibrahim Boubacar Keita, amekubali ombi la kujiuzulu kwa Waziri Mkuu Soumeylou Boubeye Maiga pamoja na baraza lake zima la mawaziri.

Soumeylou Boubeye Maiga alichukuwa hatua hiyo, jana, kufuatia wiki mbili za maandamano ya umma dhidi ya mauaji ya kiholela katika taifa hilo la Magharibi mwa Afrika.

Maandamano hayo yalichochewa na mauaji ya wachungaji 160 wa jamii ya Fulani, ambayo yanashukiwa kufanywa na watu wa jamii ya Dogon wanaoishi kwa kilimo na uwindaji.

Mauaji hayo yaliitikisa nchini humo, ambapo katika miezi ya karibuni imeshuhudia mauaji mengine kadhaa yakiwamo yale ya wanajeshi 23 walioshambuliwa kwenye kituo chao.

Hata hivyo, Soumeylou Boubeye Maiga alitangaza kujiuzulu wadhifa wake, siku moja kabla ya wabunge kupigia kura muswada wa kutokuwa na imani naye.

Hatua ya kujiuzulu kwa Maiga, imekuja baada ya wabunge wa upinzani na wale wa chama tawala cha RPM nchini humo kuwasilisha muswada wa kutokuwa na imani naye.

Muswada huo ulipigiwa kura jana, ikiwa ni ishara kuwa wabunge wengi wamekosa imani na kiongozi huyo.

Baba Dakono, ambaye ni mtafiti katika kituo cha jijini Bamako anaona kuwa kuondoka kwa Waziri Mkuu Soumeylou kutamdhoofisha Rais Ibrahim Boubakar Keita.

Maandamano ya kumtaka Waziri Mkuu kujiuzulu yalishuhudiwa siku 10 zilizopita, ambapo viongozi wa kidini na wapinzani waliandamana kumtaka aachie ngazi kutokana na kuongezeka kwa visa vya ukosefu wa usalama nchini humo. **RFI**

# Ajikata kidole baada ya kukosea kupiga kura

**NEW DELHI,** India

KIJANA mmoja nchini India, Pawan Kumar, amejikata kidole baada ya kugundua kuwa alipiga kura chama cha siasa ambacho hakukidhamiria.

Kumar akizungumza kwenye video aliyojirekodi na kuisambaza mitandaoni alisema kwa bahati mbaya alipiga kura chama tawala Bharatiya Janata (BJP).

Alieleza kuwa alitaka kukipigia chama kingine, lakini alichanganya alama nyingi zilizokuwa kwenye mashine ya kupigia kura.

Kila mpiga kura kidole chake cha shahada huwekwa alama kwa wino baada ya kupiga kura. Kumar alipiga kura yake siku ya Alhamisi katika eneo la Bulandshahr Jimbo la Kaskazini la Uttar Pradesh.

**Nilitaka kupiga kura kwenye alama ya tembo, lakini nikapiga kwenye alama ya ua kimakosa.**

"Nilitaka kupiga kura kwenye alama ya tembo, lakini nikapiga kwenye alama ya ua kimakosa," alisema Kumar kwenye video.

Alielezea kuwa alama za vyama zilikuwa kwenye mashine sambamba na jina la kila mgombea.

Uchaguzi huo ni wa awamu saba, huku kura zikitarajiwa kuhesabiwa ifikapo Mei 23. Nchini India kuna wapigakura milioni 900, inasemekana uchaguzi wa India ndiyo mkubwa kuwahi kushuhudiwa duniani.

Wakati BJP alama yake ni Ua, Tembo ni alama ya chama cha Bahujan Samaj (BSP), chama kilichoungana na vyama vingine viwili vinavyopambana na chama tawala.

Alama za vyama zina nafasi kubwa kwenye uchaguzi wa India kwa kuwa ni rahisi kutambulika kwenye nchi yoyote ambayo ina watu wengi wasio na elimu.

India kuna vyama mbalimbali na vile vya muungano ambavyo huwachanganya wapiga kura. **BBC**



Waziri Mkuu wa Mali, Soumeylou Boubèye Maïga ambaye ametangaza kujiuzulu. **PICHA: AFP**

# Wananchi Afrika Kusini kususia uchaguzi

**JOHANESBURG,** Afrika Kusini

IKIWA umebaki mwezi mmoja kabla ya wananchi wa Afrika Kusini kupiga kura kumchagua rais mpya, wakazi wa vitongoji cha Alexandra kilichopo Johannesburg wamesema watasusia kushiriki uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Mei 8.

Sababu kuu waliyoitaja ni kukosa huduma za msingi pamoja na maisha yao kuwa duni.

Wakati huo huo, Rais wa nchi hiyo, Cyril Ramaphosa, anayegombea muhula wake wa kwanza ameahidi kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya huduma za kijamii.

Lakini Rais Ramaphosa anasisitiza kuwa: "Ni lazima tujibu machungu na maisha magumu wanaoshuhudia watu wetu hapa. Hata hivyo wakazi wengi hapo hawaamini mambo yatabadilika."

Chama cha ANC kilichoko madarakani tangu uhuru wa Afrika Kusini mwaka 1994, kina viti 249 bungeni sawa na asilimia 62 ya viti 400 vya Bunge. Wakati chama kikuu cha upinzani cha DA kina asilimia 22.

Wachambuzi wa siasa wanasema kuwa bado chama cha ANC kinaamini kuwa upinzani sio tishio kwa chama tawala.

Wakati kampeni zikipamba moto kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo, wakazi wengi wa Alexandra hawana imani tena na chama tawala cha ANC, huku wengine hawana imani na chama kikuu cha upinzani cha DA kilichochukua udhibiti wa Jiji la Johanesburg tangu mwaka 2016.

Johanna Ditsela mkazi wa kitongoji hicho anasema huwenda hatopiga kura kwenye uchaguzi huo.

"Mimi ninahitaji kazi na ninahitaji nyumba kwa ajili ya watoto wangu, ili niweze kuwalea katika nyumba yenye hadhi nilikuwa na matumaini kwamba siku moja nitakapofariki nitawaachia wanangu makazi ya heshima," alisema mkazi huyo.

Mkazi iwa kitongoji hicho, Ditsela mwenye umri wa takriban miaka 50 alisema ameishi katika kitongoji hicho kwa miaka 30 katika nyumba ya mabati pamoja na watoto wake watano kando ya mtaro wa maji machafu.

NontsikeleloThinto mkazi mwingine wa kitongoji hicho alisema hata Rais Ramaphosa akiwatembelea hatoweza kuleta mabadiliko yoyote.

Ramaphosa amekuwa akihudhuria kampeni usiku na mchana akiwaomba wapiga kura milioni 27 kumpatia nafasi nyingine na kukichagua chama chake cha ANC.

Katika kampeni zake kiongozi huyo aliyechukuwa madaraka baada ya aliyemtangulia Jacob Zuma kulazimika kuacha madaraka kutokana na kashfa za rushwa mwaka 2018, amekuwa akiahidi nyumba mpya, kompyuta shuleni na maisha bora. **VOA**

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kujeruhiwa. Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji, mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua...

# KISANDUKU CHEUSI - **44**




**Na Adam Fungamwango**

GHAFLA mlango ukagongwa. Kulikuwa na aina fulani ya ugongaji ambao haukumtia wasiwasi Eddy, akafungua.

Aliyetangulia mbele ni Samson Mwakabana, Bosi Mkuu wa Usalama wa Taifa.

Nyuma yake aliongozana na maofisa wa vyeo vya juu wa polisi, pamoja na watu wengine watatu waliovalia kiraia.

"Bosi, nadhani kazi nitakuwa nimeshaimaliza. Yule pale mwenye shati ya bluu anaitwa Benson Mapunda. Huyu ndiye mhusika mkuu wa ajali ya basi la abiria iliyotokea miezi sita iliyopita huko Mikese na kuua watu zaidi ya 10, huku ikiaminiwa kuwa limeungua moto. Lakini pia ndiye mhusika mkuu wa mauaji wa watu wengine kama yule msichana aitwate Hellen mkazi wa Tabata Kimanga, Said, yule kijana mpaka kucha. Na sababu zote za mauaji ni moja tu. Alitaka kuumuua mpenzi wake Careen aliyepanda basi hilo la Bomoa Trans ili aende kuolewa na mwanaume mwingine. Lakini hawa wengine ilikuwa ni kuficha siri hiyo iliyokuwa ikikaribia kutoka."

"Vizuri Eddy, hongera kwa kazi yako nyingine nzuri, lakini kama kawaida yako huwa ukimaliza kazi kama hizi hukosi ushahidi kwa sababu tunaweza kupeleka kesi mahakamani tukakwama." Mzee Mwakabana aliongea huku akikuna upara wake.

Eddy aliingiza mfukoni na kutoa redio ya kunasa sauti, akamkabidhi bosi wake.

"Humu mna kila kitu, na ni yeye wenyewe ndiye aliyekiri kwa sauti yake, na alifanya hivyo akidhani kuwa ataniua, hivyo kabla ya kunimaliza alitaka anayemuua ajue ukweli wote kabla ya kuuawa. Lakini Bosi ushahidi mwingine nitakuja kuuwasilisha kesho ofisini kwako. Kuna mahojiano ya watu kadhaa niliofanya nao huko Ifakara kama vile shangazi ya marehemu Bi. Mkali, Nassy, na wazazi wa mume mtarajiwa wa Carren, bwana Mayambua, lakini pia CD aliyojirekodi bwana huyo kabla ya kujinyonga.

"Vizuri sana Eddy, siku zote hujawahi kuniangusha. Unajua umri wangu wa kustaafu umefika, lakini nimekuwa nikiongezewa mkataba kwa sababu yako kutokana na kazi nzuri unazofanya kwa maslahi ya taifa." Bosi huyo alisema kutoka ndani ya moyo wake, kana kwamba anamwambia mtoto wake wa kumzaa.

Kwa muda mfupi tu hali ya hewa mle ndani ilibadilika. Haikuwa nzuri tena. Kipoza hewa kilikuwa kimezimwa, hivyo mchanganyiko wa maiti tatu, ya baunsa na mwenzake, pamoja na mlinzi mmoja wa Mapunda aliyemuua mwishoni na Eddy, pamoja na mtapakao wa damu ulianza kuleta harufu mbaya.

**Ni kweli, lakini kuna baadhi ya askari wanatakiwa kubaki ili kuendelea kufanya uchunguzi kwenye hili jengo ni kwa nini limetoka kuwa godauni ya kuwekea mazao na kugeuka kuwa genge la wahalifu na wauaji.**

"Bosi nafikiri sasa tutoke humu ndani kwa sababu hali ya hewa hairuhusu tena," Eddy alishauri.

"Ni kweli, lakini kuna baadhi ya askari wanatakiwa kubaki ili kuendelea kufanya uchunguzi kwenye hili jengo ni kwa nini limetoka kuwa godauni ya kuwekea mazao na kugeuka kuwa genge la wahalifu na wauaji." Mwakabana akaongeza.

Ni muda ule ule ambao Mapunda alitiwa pingu, pamoja na walinzi wake wawili waliobaki hai na kutolewa ndani ya chumba hicho, tayari kwa kufanya mambo mawili.

Kwanza kulifahamisha Taifa ukweli wote uliotokea juu ya ajali ya Bomoa Trans na mambo yalivyoendelea hadi mwisho ili wananchi wapate kujua kuwa wakati mwingine kuna majanga hutokea wakati wakajua ni mapenzi ya Mungu kumbe si kweli, kuna mkono wa mtu.

Lakini ili kuujua ukweli inatakiwa kuwe na watu wenye upeo wa hali ya juu kama kina Eddy Kamal kuweza kubaini ukweli.

Taifa pia lijue kuwa kuna baadhi ya watu maarufu ambao kwa hali ya kawaida mbele ya wananchi na jamii wanaonekana ni watu safi, lakini nyuma ya pazia ni waovu. Na wakati mwingine hugeuzwa kuwa hivyo kutokana na sababu mbalimbali za kimaisha, ikiwamo hili la mapenzi kama lilivyomtokea Benson Mapunda. Mmiliki na Mkurugenzi Mtendaji na Hoteli kubwa nchini iitwayo Paradiso ambaye alikuwa akiheshimika na kuchukuliwa ni mmoja wa matajiri wa mfano nchini, lakini akageuka si tu kuwa muuaji, lakini pia kumuliki genge la majambazi ambao kazi yao ilikuwa kuua kila mmoja wanaomdhania anajua siri au atatoa siri ya bosi wao kumuua mpenzi wake Careen.

******************************

Alipotoka nje akiwa ameongozana na bosi wake pamoja na maofisa wengine wa usalama na askari, Eddy alishuhudia baadhi ya walinzi walikuwa wamekusanywa na kuwekwa chini ya ulinzi na askari polisi waliokuwa wametanda kwenye jengo lile.

Alijipongeza kwa uamuzi alioufanya ulimrahisishia kazi, ingawa ulikuwa ni wa hatari.

Ulikuwa ni wa kutoroka usiku wa jana chini ya ulinzi mkali ya jengo lile linalolindwa saa ishirini na nne na walinzi wenye uzoefu pamoja na juu ya ukuta kuwa na nyaya zenye umeme mkali.

Lakini alifanikiwa kutoroka na kurudi nyumbani kwake, akamwita sekretari wake Lily, pamoja na mambo mengine alimuandikia ujumbe ampelekee Bosi Mwakabana, kabla hajachukua silaha ambazo aliona zitamfaa kwa kazi yake na kurejea tena kwenye jengo lile kwa usiku huo huo mmoja bila kushtukiwa.

Ujumbe aliomuandikia ndiyo uliomfanya Mwakabana kujua aliko Eddy na anafanya nini.

Alimweleza kwa siku mbili tatu ambazo haonekani ni kwamba amejitekesha kwa watekaji kwa makusudi na huko amegundua vitu vingi, ikiwa ni pamoja na mhusika mkuu wa mauaji yaliyojitokeza hivi karibuni katika jiji la Dar es salaam, pamoja na kufahamu ukweli wote juu ya ajali ya Mikese ya basi ya Bomoa Trans.

Katima maandishi yale akamwambia bosi wake kwenye jengo ambalo yupo. Akamtaarifu kuwa wakati anaandika waraka huo alikuwa ametoroka ili kuchukua baadhi ya silaha, lakini pamoja na kupata fursa ya kumtaarifu ili awataarifu askari polisi na watu wengi wa usalama kuanzia kesho asubuhi kuanza kulifutilia jengo hilo bila wao kujua mpaka hapo atakapowataarifu kuvamia.

Alimwambia bosi wake kuwa anadhani muda wa kuanzia saa moja usiku ndiyo utakuwa mzuri wa kuanza kasheshe na akilianzisha, basi atabonyeza kitufe alichokuwa nacho na kitatoa taarifa kwake kwenye kitufe kingine alichonacho Mwakabana na yeye atawataarifu watu wake aliowaweka wakizungukia jengo hilo ili wavamie na kuwatia ndani watu wote waliokuwa humo.

Na kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi mkubwa. Wakati Eddy alipomuua yule jamaa wa kwanza aliyekwenda kumfungulia mlango ili wakammalize, alibonyeza kitufe kuonyesha tayari kazi imeanza na Mwakabana haraka akawapigia watu wa usalama waliokuwa wakisubiri mari tu, wakalizunguka jengo.

Mwakabana aliwaambia wawakamate tu walinzi na wasiingie ndani kwani alijua Eddy anashughulika, hivyo hakutaka aingiliwe.

Alichofanya ni kujiandaa na kuchukua maofisa wengine wakubwa na kuingia ndani ya gari lake moja kwa moja hadi kwenye eneo hilo. Ishara ya pili ya kengele ya kitufe ilimuashiria sasa yeye na maofisa wake waingie ndani na alipofanya hivyo alimkuta tayari Eddy ameshamaliza kazi.

"Kazi nzuri sana Eddy, nchi itaendelea kukukumbuka na kukuenzi kwa kazi kubwa unayoifanya."

Jina la Eddy lilimshtua Mapunda. Alishangaa kuona bosi yule akitamka jina la Eddy kwa askari yule mpelelezi aliyeishi naye kwenye jengo lake kwa wiki nzima.

Aligeuza kichwa chake na kutazama tena Eddy. "Kumbe huyu ndiye Eddy?" Alijiambia mwenyewe.

Alijikuta akianza kutetemeka mwenyewe. Pamoja na kukamatwa, lakini alidhani kuwa alicheza na askari mpelelezi wa kawaida. Kumbe alikuwa ni Eddy. Mpelelezi ambaye hajawahi kumuona kwa sura, lakini habari zake hakuna mtu asiyezijua. Ni mmoja wa wapelelezi hodari na hatari si tu Tanzania, bali Afrika nzima.

Anakumbuka jinsi alivyokuwa akisoma kwenye magazeti jinsi alivyoweza kukabiliana na mikasa mingi ya ajabu, lakini na kuibua mambo mazito yaliyojificha yanayopangwa na maadui wa taifa.

Alidhani alimteka Mayambua ili amuue, kumbe alikuwa amemteka Eddy. Lilikuwa ni kosa kubwa sana maishani wake.

Alizidi kujutia uamuzi wake. Wakati akipanga kulipua basi kwa ajili ya kumuua Careen, hakujua kama mambo yatakuwa makubwa kiasi cha kuingiliwa na mpelelezi mkubwa kama huyo.

Pamoja na kukamatwa kwake, kimoyomoyo alimsifu na kukubali kuwa ni mpelelezi makini na anayeijua kazi yake vema kwa sababu kama ingekuwa ni mpelelezi wa kawaida, asingepata kitu na pia angeweza kumuua kwa jinsi alivyojipanga.

*Itaendelea Jumamosi*




REAL Madrid inatarajia kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, kwa dau la pauni milioni 86 ndani ya siku chache.

# MBAPPE: RONALDO, MESSI WOTE BORA




**PARIS,** Ufaransa

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kyliane Mbappe, ameonyesha kuwakubali zaidi wakali wa soka, Cristiano Ronaldo wa Juventus na Lionel Messi wa Barcelona.

Hiyo ni baada ya kuulizwa na gazeti la France Football kuwa ni nani angemweka benchi katika kikosi cha wachezaji 11 kama angekuwa kocha.

Mbappe kupitia jarida hilo alisema yeye angewapanga wote Ronaldo na Messi wacheze pamoja.

Mbappe ameweka wazi kwa ubora wa wachezaji hao angewapanga wote na yeye kukaa benchi.

"Kama nikitakiwa kuchagua kuwa na kati ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi katika timu yangu? Nitajiweka benchi mwenyewe ili wao wote waweze kucheza kwa sababu ni bora," alisema Mbappe.

Pamoja na kuwa Ronaldo na Messi bado wanatawala vichwa vya habari vya soka kutokana na ubora wao, Mbappe ndio kinda anayetajwa kuja kung'ara na kutamba katika tuzo za Ballon d'Or.

Kutokana na ubora wake ambao amekuwa akiuonyesha, hivyo anatajwa kuwa baada ya utawala wa Messi na Ronaldo kumalizika anaweza kuwa yeye kwenye vichwa vya habari.

# Milner: Hatutakiwi kuihofia Barcelona

**LIVERPOOL,** England

KIUNGO wa Liverpool, James Milner, amesisitiza kuwa Wekundu hao wanajiamini kuelekea mchezo ujao wa nusu fainali wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona, akibainisha kwamba, hawahitaji kuwahofia miamba hao wa Katalunya.

Ushindi wa jumla wa mabao 6-1 dhidi ya Porto katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ulishuhudia Liverpool ikifuzu nusu fainali ya michuano hiyo kwa mara ya pili mfululizo.

Kwa upande wa Milner anaona kwamba, Liverpool hawapaswi kuihofia Barcelona kuelekea mchezo huo.

"Ni timu ngumu kucheza nayo. Lakini hata sisi tuna uwezo wa kufanya vizuri dhidi yao na kuweza kupata ushindi," alisema nahodha huyo msaidizi wa Liverpool.

"Kucheza pale Nou Camp ni sehemu nzuri na ninaamini tutakuwa na wakati mzuri kuwa pale. Ingawa haitakuwa kazi rahisi na tumejipanga kucheza kuhakikisha tunapata matokeo."







# *Coutinho aelezea 'staili' aliyoshangilia*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Philippe Coutinho, ameelezea sababu iliyopo nyuma ya 'staili' ya ushangiliaji wake wakati alipofunga bao kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United kwenye dimba la Camp Nou wiki hii.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alifunga bao kwa kuweka vidole masikioni mwake na kufumba macho akibeza shutuma alizokuwa akipewa kwa kushuka kiwango kwa miezi ya hivi karibuni.

Coutinho amekuwa akishutumiwa kuwa ameshindwa kufikia thamani ya euro milioni 160 alizosajiliwa nazo kutoka Liverpool na kuziba nafasi ya gwiji, Andres Iniesta.

Lakini kiwango chake kwenye mchezo wa Jumanne dhidi ya United kilikuwa moja ya kiwango bora zaidi kuichezea Barcelona na alitaka kuwaziba mdogo wale wote wanaomshutumu.

Na baadaye aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram akielezea sababu ya kuweka vidole masikioni na kufumba macho akisema: "Hatutakiwi kuwasikiliza watu ambao wanatukatisha tamaa.

"Unatakiwa kuwajibu kwa kufanya vizuri na wao watanyamaza," aliandika mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.




# ARSENAL YAMTENGEA KITITA UNAI

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery, atapata pauni milioni 75 kwa ajili ya usajili wa kipindi cha majira ya joto kama atapata nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa mujibu wa ripoti.

Arsenal ipo kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku sasa ikiwa katika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu England na imefuzu hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa.

Kwa mujibu wa Goal.com kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya hakutamwongezea fedha zaidi Emery kwa ajili ya usajili wa kipindi cha majira ya joto, ambapo hadi sasa ameshatumia kiasi cha pauni milioni 71.

Sehemu ya fedha hizo zilitumika kumsajili golikipa, Bernd Leno na kiungo Lucas Torreira.

Ripoti zinasema kwamba Emery atatumia pauni milioni 45 tu kama washikabunduki hao hawatafuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

# Mourinho awapa mbinu Tottenham kuifunga Ajax



**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho, ametoa mbinu zitakazoweza kuisaidia Tottenham kuiua Ajax inayoonekana tishio kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mourinho ametoa mbinu hizo baada ya kuulizwa swali na mwandishi wa habari kwenye mahojiano yake na kituo cha runinga cha RT Sports kuwa ni kwa namna gani Ajax anaweza kufungwa.

Ajax imekuwa timu ambayo imewashangaza wengi kutokana na kuwapiga mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Real Madrid na kuwafungisha virago katika hatua ya 16 bora, huku ikifanya hivyo kwa miamba wa soka ya Italia, Juventus yenye mchezaji, Cristiano Ronaldo kwenye hatua ya robo fainali na kufanikiwa kuingia nusu fainali ambapo itacheza na Tottenham ya England.

Baada ya vijana wa Mauricio Pochettino kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali kwa kuwafunga wababe wa Ligi Kuu England, Manchester City sasa wapata ushauri kutoka kwa Mreno huyo ambaye ameitumikia United kwa mafanikio.

Ikumbukwe kuwa Mourinho, aliweza kuiongoza United kuifunguka Ajax kwa jumla ya mabao 2-0, mwaka 2017 kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Europa na kutwaa kombe hilo, huku ikifanikiwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya moja kwa moja.

Mreno huyo anaamini anayo "fomula" itakayoweza kuwazuia vijana hao ambao wanaonekana wapo moto kwa kuwatoa Real Madrid na Juventus.

Akizungumza na RT Sport, Mourinho amesema mbinu walizotumia na kuweza kuwafunga, hivyo anaamini kama Spurs watatumia wataibuka na ushindi.

Ajax imezidi kuwa na nguvu baada ya kughairishwa kwa mechi zake zote za ligi inayoshiriki 'Eredivisie' mpaka pale itakapomaliza michezo yake ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## Sarri apuuzia shutuma dhidi yake

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri amezijia juu tuhuma anazopewa akisisitiza kwamba rekodi yake kwenye Ligi ya Europa inathibitisha kuwa yeye ni mwalimu mzuri kuweza kuiongoza timu kubwa.

Wakati wake akiwa Napoli kati ya mwaka 2015 na 2018, Sarri mara kwa mara alishindwa kufanya vizuri kwenye Ligi ya Europa na Ligi ya Mabingwa Ulaya, na wengi wamekuwa wakimnyooshea kidole kwa kushindwa kutwaa taji lolote.

Hata hivyo, akizungumza na Sky Sport Italia baada ya Chelsea kushinda 4-3 dhidi ya Slavia Prague Alhamisi, Sarri amedai kwamba rekodi yake kwenye Ligi ya Europa itazungumza yenyewe.

Alisema: "Huu ulikuwa ni mchezo wa 22 wa Ligi ya Europa na nimeshinda mara 18. Bado sitambuliki kama kocha kwenye mashindano ya Ulaya."

Aliongeza: "Sahamani kwa Napoli. Najua kwamba ni vigumu, kama ilivyo ngumu kucheza na Arsenal.



# DOND... A SOKA MAGAZ... A ULAYA



# HAZARD KUTIMIZA NDOTO ZA MADRID

## Atakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na Mfaransa Zidane kikosini hapo...

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inatarajia kukamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, kwa dau la pauni milioni 86 ndani ya siku chache.

**Mchakato wa kumsajili mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji uko katika hatua za mwisho, gazeti la Hispania liitwalo Marca limeandika.**

Endapo usajili wa Hazard utakamilika wakati wowote kuanzia sasa, atakuwa ni mchezaji watatu kusajiliwa na Real kuelekea maandalizi ya msimu mpya.

Klabu hiyo iliyokuwa inashikilia taji la Mabingwa wa Ulaya tayari imeshafikia makubaliano na Eder Militao pamoja na Rodrygo Goes, ikiwa ni chini ya Zinedine Zidane ambaye anaanza kukisuka upya kikosi chake baada ya kurejea klabuni hapo.

Kwa mara ya kwanza Zidane alishauri Real imsajili Hazard wakati mshambuliaji huyo akiwa mdogo na anaichezea Lille ya Ufaransa, na Rais Florentino Perez alisema kuwa atamnunua nyota huyo ndani ya Bernabeu wakati atakapofikia kiwango kilichopevuka zaidi.

Na ndoto hiyo sasa inaonekana kutimia kwa Real kumsajili Hazard akiwa ameshaimarika na kuwa na uzoefu wa muda mrefu.

Katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, Chelsea ilihitaji kiasi cha zaidi ya pauni milioni 170 ili kumuuza Hazard, lakini mahusiano kati ya klabu hizo mbili yalikuwa hafifu kutokana na msuguano uliotokea katika usajili wa mkopo wa nyota, Mateo Kovacic. Jambo hilo limeifanya klabu hiyo ya Hispania kuzungumza na Chelsea ili iwapunguzie dau na kufikia kiasi cha pauni milioni 86, akiwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Kitu kingine ni kuwa Chelsea imewasilisha rufani dhidi ya kifungo chake cha usajili, ikiomba kusogezwa mbele baada ya dirisha la usajili kumalizika, jambo ambalo litawasaidia kukamilisha mchakato huo kwa kuziba nafasi za wachezaji ambao wataondoka.

Tayari wameshafikia makubaliano ya kumsajili nyota, Christian Pulisic kutoka Borussia Dortmund.

## ZISIKUPITE

### PEPE KUMRITHI HAZARD

CHELSEA ambayo inatajwa itamuuza Eden Hazard kwa kiasi kidogo cha fedha, iko katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Nicolas Pepe (23), ili kuziba pengo la mshambuliaji huyo. ***(AS - in Spanish)***

### WATENGEWA FUNGU

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anatarajiwa kupewa kiasi cha pauni milioni 430 kwa ajili ya kuhakikisha anamsajili kiungo Mfaransa wa Manchester United, Paul Pogba (26) na straika wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane (27), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### BENITEZ KUPEWA NGUVU

NEWCASTLE inatarajia kumpa kocha wake, Rafael Benitez kiasi cha pauni milioni 50 kwa ajili ya kufanya usajili katika dirisha la majira ya joto, na inaamini kiasi hicho cha fedha kitamfanya Mhispania huyo aendelee kubakia klabuni hapo St James' Park. ***(Mail)***

### DEMIRBAY ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imeweka wazi nia yake ya kumsajili mshambuliaji wa Hoffenheim Kerem Demirbay (25) kwa dau la pauni milioni 22 ili kuziba nafasi itakayoachwa na kiungo wa Wales, Aaron Ramsey. ***(Metro)***

### KOULIBALY AIKANA UNITED

BEKI wa kati wa Napoli na Timu ya Taifa ya Senegal, Kalidou Koulibaly (27) amekanusha uvumi kuwa anaondoka katika klabu hiyo ya Serie A na kujiunga na Manchester United. ***(Express)***

### SPURS KUBORESHWA

MAURICIO Pochettino anatarajia kutoa kiasi cha pauni milioni 150 kukiimarisha kikosi chake cha Tottenham katika majira ya joto na anajipanga kuwauza mabeki wake wawili, Danny Rose (28) na Kieran Trippier (28). ***(Mail)***

### ARFIELD AWEKWA SOKONI

MABOSI wa Southampton wanajiandaa kumsajili kiungo wa Rangers raia wa Canada, Scott Arfield. ***(Mirror)***

### PHELAN, SOLSKJAER SAFI

KOCHA Msaidizi wa Manchester United, Mike Phelan amekiri kuwa anamshauri bosi wake, Ole Gunnar Solskjaer katika mipango mbalimbali ya usajili kuelekea kipindi cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### DZEKO: SIRUDI ENGLAND

STRAIKA wa Roma kutoka Bosnia, Edin Dzeko (33), amesema kuwa yuko tayari kujiunga na Inter Milan na hana mpango wowote wa kurejea kucheza soka nchini England. ***(Calciomercato)***

### COSTA AIGOMEA ATLETICO

STRAIKA Mhispania, Diego Costa (30), amekacha kuendelea kufanya mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake wa Atletico Madrid baada ya kufungiwa kucheza mechi nane za ligi. ***(AS - in Spanish)***

### LIVERPOOL KUIFUATA SPURS

LIVERPOOL inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya "nyumbani" katika Jiji la London katika kipindi cha majira ya joto dhidi ya Tottenham kwenye uwanja wake mpya. ***(Liverpool Echo)***

## HABARI MICHEZO



Wahitimu wa kozi ya ukocha wa mpira wa miguu ngazi ya kati, wakiwa na viongozi wa Chama cha Soka Ubungo (UFA) iliyoko jijini Dar es Salaam, ambao ndio waandaaji wa kozi hiyo. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# KMKM yaongoza kufunga Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HADI kufikia jana, jumla ya mabao 838 yamefungwa katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu Zanzibar msimu huu ambayo inaelekea ukingoni, imeelezwa.

Mabao hayo yamepachikwa katika michezo 332 ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye viwanja mbalimbali vilivyoko Unguja na Pemba.

Ligi Kuu Zanzibar ambayo inashirikisha timu 19 inaendeshwa bila ya kuwa na mdhamini mkuu kama ilivyo kwa "ndugu" zao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabaharia wa KMKM wenye mabao 78 na wako katika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ndio wanaongoza kwa kupachika mabao wakifuatiwa na Zimamoto wenye mabao 72, huku nafasi ya tatu inashikiliwa na JKU yenye magoli 62.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea leo kwa Jang'ombe Boys kuikaribisha chuoni kwenye Uwanja wa Mau "A" kuanzia saa 10:00 jioni, huku mapema mchana kwenye uwanja huo huo, Mafunzo watauamana na Zimamoto.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itawakutanisha JKU dhidi ya "Maafande" wa Polisi.



# SERIKALI YAWATAJA SPORTPESA MAFANIKIO YA MICHEZO NCHINI

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harisson Mwakyembe, ameitaja Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya SportPesa kuwa ni sehemu ya mafanikio ya michezo hapa nchini.

**Kauli hiyo aliitoa jana Bungeni wakati akiwasilisha bajeti yake ya michezo kwa wabunge wa Tanzania.**

SportPesa wanatarajiwa kuwaleta nchini mabingwa mara tano wa michuano ya UEFA Europa, Sevilla, ikiwa ni sehemu ya maandalizi yao ya msimu mpya wa 2019/2020.

Akiwasilisha bajeti hiyo, Mwakyembe alisema katika kufikia mafanikio zaidi, wizara yake itaendelea na mahusiano mazuri waliyoyaanzisha na wadau zikiwamo sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza michezo nchini.

Mwakyembe alisema SportPesa, tofauti na kukuza michezo nchini, imekuwa sehemu ya mafanikio ya miundombinu kwa kuweka nyasi mpya za bandia na kusimamia utunzaji wake kwa kipindi cha miaka miwili. Aliongeza kuwa, pia SportPesa imefanikisha kuandaa mashindano ya SportPesa Cup ambayo yamekuwa yakifanyika hapa nchini kwa mara mbili tangu kuanzishwa kwake 2017.

"Yapo mafanikio mengi ya michezo yamepatikana ndani ya kipindi hicho na hayo yametokana na wizara yangu kuwa na uhusiano mzuri na sekta binafsi na baadhi ya kampuni.

"Kati ya kampuni hizo, ipo SportPesa ambayo imefanikisha kuandaa michuano ya SportPesa tangu mwaka 2017 na Tanzania imefanyika kwa muda wa miaka miwili tangu kuanzishwa kwake.

"Pia, SportPesa imesaidia kuweka miundombinu mizuri hapa nchini mfano ilifanikisha uwekaji wa nyasi bandia mpya kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam, huku ikitumia miaka miwili katika utunzaji wake.

"SportPesa ilifanikisha ziara ya ujio wa klabu ya Everton ya England hapa nchini na tena mapema wiki hii imetangaza kuileta Sevilla," alisema Mwakyembe.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 3. Simba | 23 | 19 | 3 | 1 | 50 | 8 | 60 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 11. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 13. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 32 | 8 | 12 | 12 | 26 | 34 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# *Makocha wapya Ubungo wafundwa*

**Na Mwandishi Wetu**

WAHITIMU wa kozi ya ukocha wa mpira wa mguu ngazi ya kati, wametakiwa kuhakikisha wanapata klabu za kufundisha ili kutumia kwa vitendo elimu waliyoipata kwa ajili ya kukuza kiwango cha mchezo huo hapa nchini.

Jumla ya wahitimu 42 wa kozi hiyo walikabidhiwa vyeti baada ya kumaliza kozi hiyo iliyoandaliwa na Chama cha Soka Wilaya ya Ubungo (UFA) iliyoko jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na wahitimu hao, Mkufunzi wa Makocha wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Bundala, aliwaambia wahitimu hao kuwa "kukalia" elimu hiyo waliyoipata watakuwa hawajitendei haki na vile vile watashindwa kusaidia maendeleo ya soka ambayo yanahitaji nguvu za wadau mbalimbali.

Bundala alisema pia idara yake haitawapa nafasi makocha wasiokuwa na timu kuendelea kushiriki kozi mbalimbali zinazoandaliwa kwa sababu watakuwa hawatekelezi sera za kutengeneza vipaji kama ambavyo TFF na UFA inavyowatarajia.

Alisema pia ameridhishwa na mwamko mkubwa wa makocha waliojitokeza kushiriki kozi hiyo kwa sababu wanataka kuona timu au vituo vyote vinavyofundisha soka kutumia walimu ambao wamepata mafunzo rasmi.

"Kuwekeza katika walimu ndio jambo kubwa, hakuna njia nyingine itakayotutoa kama hujawekeza kwenye elimu, inasaidia kuinua vijana na hapo tutapata maendeleo tunayoyalilia," alisema mkufunzi huyo.

Ahmed Prezidaa, mmoja wa wahitimu wa kozi hiyo alisema kuwa amejifunza vitu mbalimbali muhimu katika soka ambavyo huko nyuma alikuwa hazifahamu.

"Ni darasa ambalo limetubadilisha, tumeongeza madini katika vichwa vyetu, haikuwa kazi rahisi, lakini tunamshukuru Mungu tumemaliza salama," alisema Prezidaa.

Michezo
Jumamosi Aprili 20, 2019
Nipashe



Hazard kutimiza ndoto za Madrid UKURASA 30

# Kocha Serengeti Boys: Tunaweza

**Na Mwandishi Wetu**

WENYEJI timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) inatarajia kukwakabili yosso wenzao kutoka Angola katika mechi ya mwisho ya Kundi A ya Fainali za Afrika (AFCON U-17) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ambayo ni ya "Do or Die" kwa Serengeti Boys itacheza kuanzia saa 10:00 jioni sawa na mchezo mwingine wa kundi hilo utakaowakutanisha Nigeria na Uganda kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Serengeti Boys wanahitaji kupata ushindi mnono ili waweze kusonga mbele katika michuano hiyo au kumaliza kwa heshima kutokana na kupoteza mechi zake mbili za awali ambazo walicheza dhidi ya Nigeria na Uganda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Oscar Mirambo, alisema kuwa amewaandaa vema na wachezaji wake tayari kupambana ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wa leo.


Mirambo alisema kuwa hawajakata tamaa ya kusonga mbele katika mashindano hayo kwa sababu anaamini lolote linaweza kutokea katika mchezo wa leo dhidi ya Angola ambao wana pointi tatu mkononi.

"Tunaamini kwenye nafasi ambayo ipo, nani anajua, timu ya wakubwa ilifuzu katika mchezo wa mwisho, huku ikitegemea pia mechi nyingine, chochote katika mpira wa miguu kinaweza kutokea, kitu cha muhimu ni kushinda mechi iliyoko mbele yetu," alisema Mirambo.

Alisema kuwa alijaribu kuangalia makosa na kuwahamasisha wachezaji wake kujituma zaidi katika mechi ya leo na kuwaachia mashabiki nafasi yao ya kuendelea kuwashangilia.

Mechi za hatua ya makundi za mashindano hayo zinatarajiwa kukamilika kesho kwa Guinea kuwavaa Morocco, wakati Cameroon watachuana na Senegal.

Timu nne zitakazomaliza katika nafasi za juu zitatinga hatua ya nusu fainali na pia zitakuwa zimekata tiketi ya kushiriki Fainali za Dunia za Vijana zitakazochezwa huko Brazil baadaye mwaka huu.



Straika wa Chelsea, Olivier Giroud (kulia), akikabwa na beki wa kati wa Slavia Prague, Michael Ngadeu-Ngadjui katika mechi ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Stamford Bridge jijini London. Chelsea ilishinda mabao 4-3 na kusonga mbele. **PICHA: MTANDAO**

# Simba: Kagera Sugar itachakaa

## Maxime atangaza kuwasimamisha katika mbio za ubingwa ili kujinusuru...

**Na Somoe Ng'itu**

SIKU nane za jasho la damu kwa mabingwa watetezi, Simba ndani ya mikoa ya Kanda ya Ziwa zinatarajia kuanza leo kwa kuwavaa wenyeji Kagera Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

**Kundi la kwanza la wachezaji 18 wa Simba liliwasili Bukoba salama jana, mchana na jioni kikosi hicho kilifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Kaitaba, ambao una nyasi bandia na nyota wake wanne wengine wakitarajiwa kufika leo.**

Baada ya mechi ya leo, Simba itaelekea jijini Mwanza kuwafuata Alliance FC na KMC, halafu itasafiri tena kwenda Musoma kuvaana na wenyeji Biashara United, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Karume ifikapo Aprili 27, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, aliliambia gazeti hili kuwa wanatarajia matokeo ya ushindi, lakini wanafahamu kikosi chake kitakuwa na kazi ngumu ya kuhakikisha wanashinda katika mchezo huo.

Aussems alisema kuwa Kagera Sugar ni moja ya timu zinazotoa ushindani kwenye ligi hiyo, na nafasi waliyonayo katika msimamo wa ligi hiyo utawafanya waingie uwanjani wakiwa washindani zaidi.

Alisema si mechi yao ya leo tu, lakini mechi zote za ligi hiyo zilizosalia zitakuwa na changamoto kwa sababu makocha na wachezaji wanahitaji kutimiza malengo ya klabu zao kwa msimu huu.

"Itakuwa mechi ngumu na yenye ushindani, sisi tumejiandaa na hili na hakuna ambaye anatarajia mteremko, mechi zote tunazocheza ni ngumu, tofauti ni aina ya mashindano tu," alisema Mbelgiji huyo ambaye katika msimu wake wa kwanza amefanikiwa kuipeleka Simba kwenye hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema mchezo wa leo utakuwa na ushindani kwa sababu kila upande hauko salama katika malengo ambayo wanayo.

"Tumejipanga kuisimamisha Simba, wanatujua na sisi tunawajua vema, huwa hawanisumbui hawa, tunahitaji pointi tatu ili tupande katika msimamo, hatuko vizuri, nafasi yetu haifurahishi kama kocha siridhiki hapa tulipo," alisema Maxime, beki na nahodha huyo wa zamani wa Taifa Stars.

Simba yenye pointi 60 na imecheza mechi 23 iko katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakati Kagera Sugar ambao wako katika nafasi ya 17 wana pointi 36, lakini wameshuka dimbani mara 32.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002